# Nipashe

Jumamosi Desemba 16, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581526

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Operesheni** uhamisho Ngorongoro kuendelea

UKURASA 3

**Rungu** la Samia lavunja taasisi, mashirika 20

UKURASA 4



**Madereva** wa bajaji wagoma madai kupinga kunyanyaswa

UKURASA 5



**JEZI ZA MESSI ZAUZWA KWA MAMILIONI**

UKURASA 21



TAFSIRI KISHERIA

# Ubunge kina Mdee batili

• **KAULI** ya wanasheria, wadau baada ya uamuzi wa Mahakama, Bagonza atia neno... *Ukurasa 2*

## Wanandoa ardhi wasimamishwa kwa tuhuma za dhuluma kiwanja

UKURASA 3

# Maiti ya mtoto mchanga yamponza mganga mkuu

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi akipokea mfano wa ramani ya mji mpya wa biashara, Nyamanzi Wilaya ya Magharibi "B" Mkoa wa Mjini Magharibi kutoka kwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban Ikulu Jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

**MICHEZO** **SIMBA YAREJEA NAFASI YA TATU LIGI KUU** UK.24

**MAONI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Maiti ya mtoto mchanga yamponza mganga mkuu

**Na Augusta Njoji,** KAGERA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amemwagiza Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo kutengua nafasi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera.

Hatua hiyo ni kutokana na madai ya utendaji wake kutoridhisha ikiwamo kutochukua hatua kwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa iliyoko Bukoba, iliyozuia maiti ya mtoto mchanga.

Wakati akiagiza hatua hizo kuchukuliwa, Mchengerwa ameapa kuwashughulikia viongozi wa kisiasa na serikali ambao wamekuwa chanzo cha kukwamisha miradi ya maendeleo na kutishia kusitisha vikao vya Baraza la Madiwani Manispaa ya Bukoba iwapo litabainika kikwazo kwa maendeleo.

Alisema hayo jana katika hafla ya utiaji saini mikataba ya usanifu wa miradi ya uboreshaji miundombinu ya miji ya Tanzania (TACTIC) kwa miji 15 ya kundi la pili mjini hapa.

"Nimepata taarifa moja ya hospitali zetu mtoto amefariki dunia wamekaa zaidi ya siku mbili hawataki kuachia maiti ya mtoto mchanga huku wakijua anapaswa kuhudumiwa bure na maiti yake anapofariki aruhusiwe kwenda kuzikwa. Utoaji wa huduma lugha mbovu umeenea katika hospitali ya mkoa. Hili sitakubali hata kidogo. Nakuelekeza Katibu Mkuu kutengua mara moja nafasi ya mganga mkuu wa mkoa," alisema huku akisisitiza kuwa ni dhamana, mtu akishindwa kuwahudumia Watanzania hafai kwenye nafasi na ataondolewa.

Kuhusu maendeleo ya Bukoba, alisema kuna maeneo hawafanyi vizuri kwenye miradi kwa sababu kuna viongozi wa serikali wanaweka mikono yao.

"Viongozi wengine wanaweka mkono, wanatafuta makandarasi wao, miradi inakwama na haijengwi inavyotakiwa. Sasa nataka niwaambie wazi kiongozi yeyote wa serikali anayewajibika chini ya TAMISEMI atakayeweka mkono kwenye miradi hii ambayo Rais anataka kuwakwamua wananchi, nitashughulika naye.

"Bukoba imefika hapa ilipo kwa sababu kuna watu hawatamani kuona maendeleo kwa sababu ya maslahi yao ya kisiasa, tena wengine viongozi ndani ya serikali," alisema huku akiapa kuwa katika utekelezaji wa miradi hiyo, hatakubali kufumbia macho yeyote atakayethubutu kuikwamisha.

Alisema soko na stendi mkoani Kagera ni miundombinu ya muda mrefu tangu vita vya Kagera mwaka 1978/79 lakini sasa itajengwa ya kisasa.

Mchengerwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan amemfuta machozi Mbunge wa Bukoba Mjini, Stephen Byabato, ambaye hivi karibuni alipiga magoti na kuangua kilio akiomba ujenzi wa miradi ya soko, stendi, barabara na kujenga kingo kwenye Mto Kanoni ili kuondokana na kero ya mafuriko.

**MIRADI KUWANG'OA MA-DED**

Mchengerwa alisema mkurugenzi wa halmashauri atakayeshindwa kukamilisha kwa muda uliopangwa ujenzi wa shule kupitia fedha za BOOST na SEQUIP ifikapo Desemba 31, mwaka huu, atapendekezwa kwa Rais aondolewe kwenye nafasi yake.

"Nendeni mkasimamie miradi fedha zimetolewa, sitegemei kusikia kuna mkurugenzi ambaye ameshindwa kutekeleza miradi katika maeneo yake," alisema.

Akitoa maelezo ya mradi wa TACTIC, Mratibu wa Miradi ya Ushirikiano wa Benki ya Dunia na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Mhandisi Humphrey Kanyenye, alisema mradi unagharamiwa na serikali kuu kwa Sh. trilioni moja kupitia masharti ya nafuu ya mkopo kutoka Benki ya Dunia na utanufaisha miji 45.

"Mradi utatekelezwa kwa miaka sita kuanzia mwaka wa fedha 2022/23 lengo kuu ni kuboresha usimamizi wa ukuaji wa miji pamoja na kuwezesha halmashauri za miji na majiji kutoa huduma bora kwa wananchi. Maeneo ya utekelezaji ni ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwamo barabara na miundombinu mingine kulingana na vipaumbele vya halmashauri husika," alisema.

Alisema kundi la kwanza linahusisha miji 12 ya Mwanza, Mbeya, Arusha, Dodoma, Morogoro, Kahama, Kigoma, Songea, Sumbawanga, Tabora, Geita na utekelezaji wake umeanza mwaka huu wa fedha 2023/24.

Kundi la pili, alisema litahusisha miji 15 ya Tanga, Korogwe, Moshi, Kibaha, Iringa, Bukoba, Singida, Bariadi, Shinyanga, Musoma, Lindi, Mpanda, Njombe, Mtwara na Babati na utekelezaji wake utaanza mwaka ujao wa fedha 2024/25 baada ya usanifu kukamilika.

"Kundi la tatu linahusisha Miji 18 ya Kasulu, Tunduma, Vwawa, Ifaraka, Masasi, Nanyamba, Handeni, Bagamoyo, Mafinga, Tarime, Chato, Bunda, Mbinga,Mbulu, Nzega, Kondoa, Newala ambao utekelezaji utaanza mwaka 2024/25,"alisema.



Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, akizindua kitabu cha historia ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT). Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi ya NIT, Prof. Ulingeta Mbamba na kulia ni mwandishi wa kitabu hicho, Ramadhani Sawaka. **PICHA: NIT. Habari Uk. 4**

# Wanasheria wasema ubunge kina Mdee batili

**Restuta James na Maulid Mmbaga**

WANASHERIA na wasomi wamesema ubunge wa Halima Mdee na wenzake 18 ni batili kutokana na mahakama kubariki uamuzi wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuwavua uanachama.

Maoni hayo waliyatoa jana ikiwa ni siku moja baada ya Mahakama Kuu, Masjala Kuu ya Dar es Salaam kukubali kwamba uamuzi wa Kamati Kuu ulikuwa sahihi lakini ikatengua uamuzi wa Baraza Kuu la chama hicho kuwavua uanachama.

Wakili wa Kujitegemea, Alloyce Komba, alisema wabunge hao hawana sifa za kuwapo bungeni kwa kuwa walishavuliwa uanachama, ambayo ni sifa muhimu ya kuwa mbunge.

Alisema hukumu ya mahakama haitekelezeki kisiasa kwa kuwa mlolongo wa kufanya uamuzi ulivyo ndani ya CHADEMA, ndivyo ulivyo kwenye vyama vingine vya siasa kikiwamo Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Wanasheria wengine tunahoji kama Jaji aliona huu upungufu kwa nini hajafuta uamuzi hadi wa Kamati Kuu? Kwa mtazamo mwingine wa kisheria ni kwamba vyama vyote vya siasa vimeundwa kwa mfumo huo. Mtu anafukuzwa na Kamati Kuu, Halmashauri Kuu au Mkutano Mkuu ambao mwenyekiti wa vikao vyote ni mmoja," alisema.

Alitoa mfano kuwa ndani ya CCM waliwahi kuvuliwa uanachama makada kadhaa, wakiwamo aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernad Membe na Sophia Simba. Alisema uamuzi huo ulifanywa na viongozi kwa mfumo uliofanywa kwa Mdee na wenzake.

"Ni dhahiri kwamba tangu walipovuliwa uanachama na taarifa ikaenda kwa Spika wa Bunge, ilitakiwa akubali kwamba hawa hawapaswi kuwa wabunge, chama kimeamua.

"Kwa mtazamo wangu, Jaji ameangalia kisheria sana lakini kisiasa ndani ya vyama huo uamuzi hautekelezeki. Hata hao akina Halima wakirudi kwenye baraza hawawezi kupata haki kwa sababu waliowavua ni wajumbe wa Baraza Kuu kimfumo," alisema.

Wakili Komba alisema kama nchi, yanahitajika mabadiliko makubwa ya sheria na kwamba ikiwezekana liundwe baraza la kusimamia vyama vya siasa ili wanachama wanapokutana na changamoto ndani ya vyama, wakalalamike huko badala ya kwenda mahakamani.

Alishauri kuwa ifunguliwe kesi kuishtaki serikali kwa kuwalipa wabunge wasio halali ndani ya Bunge ili mahakama itoe uamuzi.

Mwanasheria Chali Rajabu alisema kitendo cha wabunge hao kuendelea kushiriki vikao vya Bunge ni kinyume cha utaratibu kwa kuwa chama chao hakiwatambui kutokana na ukweli kwamba walishavuliwa uwanachama.

"Mahakama pia inapaswa iliangalie hilo na itoe kauli kwamba wakae pembeni wasishiriki shughuli yoyote ya Bunge hadi pale mgogoro wao utakapoisha," alisema Rajabu.

**BAGONZA ATIA NENO**

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, Dk. Benson Bagonza, alisema baada ya hukumu hiyo, mambo matatu yanaweza kufanyika ikiwamo kuwatimua bungeni.

"Bunge litekeleze Uamuzi wa Kamati Kuu ya CHADEMA kwa kuwaondoa bungeni kwa kuwa si wanachama. Pili, mchakato wa maridhiano kati ya wabunge hao na chama chao na tatu, anayedhani ameonewa na hukumu hii akate rufani panapohusika, bado kuna nafasi ya kwenda juu zaidi," alisema.

Juzi, Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam ilitengua uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA, kuridhia uamuzi wa Kamati Kuu ya chama hicho kuwavua ubunge Halima Mdee na wenzake 18.

Baraza hilo lililosikiliza rufani ya wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia chama hicho, lilibariki wabunge hao kuvuliwa uanachama wa CHADEMA uliofanywa na Kamati Kuu ya chama hicho.

Hata hivyo, Mahakama Kuu ilisisitiza kuwa haijafuta uamuzi wa Kamati Kuu ya kuwavua uanachama Mdee na wenzake 18 kwa sababu walipewa nafasi ya kujieleza kwenye kamati hiyo, lakini hawakutumia.

Uamuzi huo ulitolewa juzi na Jaji Cyprian Mkeha wa mahakama hiyo, aliyeanza kwa kutoa ufafanuzi kwamba anajua watu wengi, wakiwamo mawakili, walikuwa wanafuatilia shauri hilo ili kujua kama ubunge wa wabunge hao ni halali au si halali.

Mdee na wenzake 18, katika suala hilo hilo walikuwa wanalalamika kwamba Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika walishiriki kikao cha Kamati Kuu kisha kushiriki kikao cha Baraza Kuu la chama kilichobariki wao kuvuliwa uanachama.

Baada ya hukumu hiyo, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, alisema chama hicho kinakaa na mawakili wake kutafsiri hatua za kuchukua kutokana na uamuzi huo wa mahakama.

"Tunamkumbusha Spika wa Bunge kuhusu utekelezaji wa uamuzi wa Kamati Kuu ya CHADEMA ya Novemba 27, 2020, ya kuwavua uanachama kwani mahakama imethibitisha kuwa walishafukuzwa uanachama kihalali na taratibu zote zilifuatwa," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Operesheni uhamishaji wananchi Ngorongoro kuendelea

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSEMAJI Mkuu wa serikali Mobhare Matinyi, amesema oparesheni ya kuwahamisha kwa hiari wananchi wa Ngorongoro mkoani Arusha wanaoishi ndani ya eneo la hifadhi itaendelea siku chache zijazo.

Amesema kampeni hiyo inatarajia kuanza na kaya 500 ambazo tayari zilishajiandikisha na kufanyiwa uthamini wa mali zao.

Aidha, kuhusu maafa yaliyotokea katika mji wa Katesh, Hanang mkoani Manyara, amesema kwa siku mbili mfululizo hakuna miili zaidi iliyopatikana kutokana na mafuriko, hivyo idadi ya waliofariki dunia inabakia 89 hadi sasa.

"Naomba nichukue nafasi hii kuzungumzia kuhusu maendeleo ya awamu ya pili kuwahamisha kwa hiari wananchi wa tarafa ya Ngorongoro wilayani Ngorongoro mkoani Arusha, wanaoishi ndani ya eneo la hifadhi ya Ngorongoro.

"Zoezi hilo litaendelea siku chache zijazo likianza na kaya 500 ambazo tayari zilishajiandikisha na kufanyiwa uthamini wa mali zao," alisema Matinyi

Alisema wanatarajia sehemu ya mradi wa nyumba 5,000 zinazojengwa katika vijiji vya Msomera wilayani Handeni (Tanga), Kitwai wilayani Simanjiro (Manyara) na Saunyi wilayani Kilindi (Tanga) itakamilika hivi karibuni.

Matinyi alisema tayari nyumba 503 zilishajengwa na kuwezesha kaya 551 kuhamia zikiwa na watu 3,010 na mifugo 25,521 na zote zipo kijijini Msomera.

"Aidha, ni vyema kufahamu kuwa kaya 27 zenye watu 120 na mifugo 769 tayari zilishahamia kwenye maeneo mengine nje ya hifadhi lakini si katika maeneo yaliyotengwa na serikali," alisema.

Pia alisema kaya hizo zilikwenda katika wilaya za Karatu, Meatu, Monduli, Simanjiro, Handeni na mkoani Arusha.

"Hawa pia walisafirishwa na kulipwa fidia na malipo ya ziada kwa kila kaya inayohamia katika maeneo yaliyotengwa na serikali inapata malipo ya fidia Sh. 10,000,000 za ziada kwa maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, inasafirishiwa yenyewe pamoja na kila kitu chake.

"Inapewa nyumba ya vyumba vitatu kwenye eneo la ekari 2.5 pamoja na hati miliki, inapewa shamba la ekari 5 pamoja na hati miliki, inapewa eneo la kuchungia mifugo la jumla kwa wote pamoja na huduma za majosho na mabwawa ya kunyweshea mifugo," alisisitiza Matinyi.

Pia alisema serikali inajenga mnada wa mifugo wa kisasa, vituo vya kununulia maziwa, shule za msingi na sekondari, zahanati na vituo vya afya, barabara, na usalama kwa wananchi wote kwa kuweka vituo vya polisi.

Matinyi pia alisema serikali inaendelea kusisitiza kwamba uhamishaji huo ni wa hiari na wananchi waepukane na taarifa potofu kuwa kuna uvunjwaji wa haki za binadamu na uondoaji watu kwa nguvu.

Kuhusu maafa ya maporomoko ya tope, mawe, magogo na maji kutoka Mlima Hanang, yaliyotokea alfajiri ya Desemba 3, mwaka huu, alisema kwa siku ya pili mfululizo hakuna miili zaidi iliyopatikana na hivyo idadi ya inabakia kuwa 89.

"Watu wazima 50, wanaume 21 na wanawake 29, na watoto 39, kiume 19 na kike 20, miili 87 imetambuliwa na kuchukuliwa na familia zao kwa ajili ya mazishi lakini miili miwili ya watoto wa kike wa umri wa mwaka mmoja na miaka mitatu, inahitaji vipimo vya vinasaba (DNA) ili kujiridhisha na utambuzi wake," alisema

Alisema idadi ya majeruhi inaendeelea kupungua ambapo sasa wamebakia majeruhi 14 kutoka 139 waliofikishwa hospitalini baada ya maafa kutokea na waathirika 36 ndio waliobakia kambini.

# Watumishi ardhi wanandoa wasimamishwa madai ya kumdhulumu kiwanja mwananchi

**Na Waandishi Wetu**



WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (pichani) , amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuwasimamisha kazi wanandoa Salvatory Rutaba na Revina Kayanda, ambao ni watumishi wa sekta ya ardhi mikoa ya Mwanza na Simiyu kwa tuhuma za kudhulumu kiwanja cha Damas Kamani kilichoko Ilemela, Mwanza.

Waziri Silaa alitoa agizo hilo jana baada ya kupokea barua ya malalamiko kutoka kwa Kamani akitaja eneo lake lililoko Mtaa wa Nyamohongolo, Ilemela, kumegwa viwanja viwili namba 863 na 864 vinavyomilikiwa na watu wasio halali.

"Baada ya kufika hapa imebidi kutumia siku tatu kufuatilia mgogoro huu na cha kushangaza nimebaini kuwa watumishi hawa ndio waliomsaidia mmiliki ambaye kwao ni wa awali, Daud Malifedha, kupata hati ya viwanja hivi.

"Nyaraka zake zinaonyesha aliomba hati ya kiwanja kimoja namba 863 mwaka 2015 wakampatia ya viwili ambacho ni 863 na 864 na kutiwa saini na Levina aliyekuwa Ofisa Ardhi Wilaya ya Ilemela ambaye baadaye alikuwa mmiliki yeye na mume wake, hali inayoleta utata," alisema.

Waziri Silaa alisema katika mgogoro huo, jambo linalotia shaka ni mchakato wa umilikishaji kutoka kwa mmiliki wa asili kwenda kwa malifedha kisha kwenda kwa wawili hao.

Alisema mchakato wake umeanzia katikati na aliyemtambulisha Malifedha katika kiapo cha uraia ni Rutaba aliyekuwa pia ni Ofisa Ardhi wa Manispaa ya Ilemela na sasa ni Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Simiyu.

Waziri Silaa alimwagiza Mkuu wa Wilaya Ilemela, Hassan Masala, kuunda timu ya uchunguzi wa mgogoro huo itakayochunguza mchakato mzima kuanzia mwaka 2019 pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara kufuta upimaji mpya uliofanyika mwaka 2019.

"Afute mchoro wa mipango miji urejewe upya ili kupata barabara inayokwenda chini kwa kutumia vipimo vya mwanzo za 2012 ili isitokee mtu akaingia kiwango kingine," alisisitiza.

Akiwa wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Waziri Silaa aliwatangazia kiama maofisa ardhi watakaobainika kutoa hati miliki kwenye kiwanja kimoja kwa watu wawili na kuahidi kuwachukulia hatua za kisheria.

"Kliniki hizi za ardhi zimefunguliwa mikoa yote ya Tanzania Bara na lengo lake ni kutatua migogoro ya ardhi wanayokutana nayo wananchi.

"Katika malalamiko 10 yanayofika ofisi za wakuu wa wilaya na mikoa saba ni ya ardhi, kati ya hayo matano ni wananchi wenye zaidi ya miaka mitano wanahangaika kupata haki zao," alisema.

Waziri Silaa alimtaka Katibu Mkuu wa Ardhi, Naibu katibu Mkuu, Naibu Waziri pamoja na watendaji wengine kuhakikisha mmoja wao anashiriki katika kliniki za ardhi wakati zinaendeshwa ili kutatua migogoro inayohitaji maelezo ya kitaifa.

Kamishna Msaidizi wa Ardhi mkoani Shinganga, Leo Komba, alikiri Mkoa wa Shinyanga kuwa na migogoro mingi ya ardhi na zaidi ya wananchi 100 wamesikilizwa na bado wanaongezeka.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alikili ofisi yake kupokea migogoro mingi ya ardhi na ile inayohitaji kuendeshwa kisheria huielekeza katika Mahakama ya Ardhi.

Mboni aliomba huduma hiyo ifike halmashauri ya Msalala na Ushetu ambako pia, kumekuwa kukiripotiwa malalamiko ya ardhi.

**•Imeandaliwa na Vitus Audax(MWANZA) na Shaban Njia (KAHAMA)**


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| BUGURUNI | EUSTACK SAMMA MSOKA | GARI HINO LIESSE II T559 DXZ | EUSTACK SAMMA MSOKA | POSTA HOUSE-ILALA | 30/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | YUSUPH JULIAS MWAKIPESILE | NYUMBA | ERASTO KAMANI | PUGU-ILALA | 29/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | BIMLA ELECTRICAL SUPPLIES | VIWANJA VIWILI | RAJABU SIMEO MAJIGE | BUIGIRI- CHAMWINO | 28/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | MARIA JOSEPH UTONGA | NYUMBA | MARIA JOSEPH UTONGA | BWAWANI HOMBOLO | 30/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | ANOLD ANTONY MIKA | NYUMBA | ANOLD ANTHONY MICHAEL | NKUHUNGU DODOMA | 29/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | INOCENCIA JANUARY LUBINGA | NYUMBA | PETRO JOSEPH MASADU | MSISI-DODOMA | 29/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | ZEPHANIA MATHAYO MBATA | NYUMBA | ZEPHANIA MATHAYO MBATA | MSISI-DODOMA | 30/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | JANVIER VOSTER LUBINGA | NYUMBA | JANVIER VOSTER LUBINGA | MSISI-DODOMA | 30/12/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | EDWARD WAMI KATEI | NYUMBA | EDWARD WAMI KATEI | MSISI-DODOMA | 30/12/2023 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 19/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0714939933/0754497396**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.




Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu (kulia) akibadilishana Mikataba na Mhandisi wa Kampuni ya China Communications Construction, Chen Jian( kushoto ) mbele ya Waziri wa Maji , Juma Aweso, wakati wa hafla ya Utiaji Saini kwa ajili ya utekelezaji miradi ya usambazaji maji maeneo matatu ya Pangani, Kwala na Kibada-Chuo cha Uhasibu wenye thamani ya zaidi ya bilioni 48 mkoani Pwani jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Rungu la Samia lafuta mashirika 20

**Na Restuta James**

SERIKALI imefuta, kuunganisha na kuvunja mashirika na taasisi zake 20, kwa lengo la kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuipunguzia serikali mzigo wa uendeshaji.

Miongoni mwa taasisi zilizoguswa ni Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Bodi ya Chai, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

Pia serikali imeifuta bodi moja, Shirika la Uzalishaji la Jeshi la Polisi (TPSCF), taasisi tatu za utafiti na Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC). Utekelezaji wa hatua ya kufuta na kuunganisha taasisi hizo, utakamilika kabla ya Julai, mwakani.

Akitangaza uamuzi huo jana jijini Dar es Salaam, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema hatua hiyo ni kutokana na marekebisho na maboresho yanayoendelea katika mashirika yote ya umma.

Kwa mujibu wa Prof. Mkumbo, mashirika 16 yaliyounganishwa yalikuwa na mwingiliano na mfanano wa malengo na majukumu huku manne yakivunjwa na kufutwa.

Alisema RITA na NIDA zimeunganishwa, hivyo itaundwa taasisi moja itakayohusika na utambuzi wa matukio muhimu kuanzia kuzaliwa hadi kufariki dunia na kwamba hatua hiyo ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwa na namba moja ya utambulisho.

Alisema TADB imeunganishwa na Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) ili kuwa na taasisi moja itakayohusika na mikopo na ugharamiaji wa maendeleo ya kilimo wakati Bodi ya Chai Tanzania imeunganishwa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania ili kuwa na bodi moja ya chai.

Pia alisema Bodi ya Nyama imeunganishwa na Bodi ya Maziwa ili kuunda taasisi moja ya kuendeleza na kusimamia mazao ya mifugo. Shughui za SIDO zimeunganishwa na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CARMARTEC) na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) ili kuunda taasisi moja.

Kuhusu TIC na EPZA, alisema zimeunganishwa ili kuunda taasisi itakayoratibu uwekezaji wa sekta binafsi wa ndani na kutoka nje ya nchi. Pia alisema na kwamba taasisi za utafiti wa chai, tumbaku na kahawa zimeunganishwa na kuwa sehemu ya muundo wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

Kadhalika, alisema Bodi ya Pareto imefutwa na shughuli zake zitahamishiwa katika Mamlaka ua Usimamizi wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko.

Mashirika yaliyovunjwa kwa mujibu wa Waziri Mkumbo, ni Shirika la Elimu Kibaha ambalo lilikuwa linamiliki sekondari ya Kibaha, Hospitali ya Tumbi na chuo cha ufundi.

Kutokana na mabadiliko hayo, hospitali ya Tumbi itakuwa chini ya Wizara ya Afya wakati sekondari ikipelekwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na chuo kikipelekwa Wizara ya Elimu.

SABABU YA HATUA

Prof. Mkumbo alisema: "Haya ni mageuzi endelevu ya uboreshaji wa mashirika ya umma kwa lengo ya kuyawezesha yajiendeshe kwa faida. Serikali itaendelea kupunguza mzigo wa kuyaendesha mashirika ya umma yanayohitaji ruzuku ya serikali katika kujiendesha."

Waziri alisisitiza kuwa: "Serikali inataka ibaki na mashirika ya umma ambayo majukumu yake hayatekelezeki bila ruzuku akitolea mfano wa shule za umma. Mashirika ya umma yanaelekezwa kuwekeza kwenye maeneo ya kimkakati kulingana na majukumu yao.

"Maeneo ambayo yanaweza yakafanywa na sekta binafsi tunataka iachiwe ifanye lengo ni kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara hapa nchini. Yale maeneo ambayo kikawaida hayavutii sekta binafsi kuwekeza lakini ni muhimu kwa uchumi wetu, serikali itajikita huko."

Waziri Mkumbo ambaye aliambatana na Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu na Katibu Mkuu wa Wizara yake, Dk. Tausi Akida, alisema serikali itaendelea kutathmini kazi za mashirika yake na kuchukua hatua stahiki.

"Nikizungumzia utafiti, kwa asili yake hauvutii sekta binafsi, hili ni jukumu la umma, kwa hiyo yapo maeneo ambayo taasisi zinapokea ruzuku hatutazilaani kwa sababu zinazoa huduma muhimu zinazohitajika kwa maendeleo ya nchi," alisema.

"Mnapaswa kuyahoji haya mashirika, mfano hili shirika linauza maziwa, hivi kweli ni lazima maziwa yauzwe na umma? Tunataka biashara inayoweza kufanywa na sekta binafsi ifanywe ili kodi za Watanzania zielekezwe kwenye maeneo ambayo kwa kawaida haiwezi kufanya sekta binafsi, kama kutoa elimu, afya na kujenga miun-

## NIT yapongezwa kuanzisha kozi urubani

**Na Prosper Makene**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, amekipongeza Chuo Cha Taifa ca Usafirisaji (NIT) kwa kuanzisha mafunzo ya marubani wa ndege.

Kikwete alitoa pongezi hizo jana katika maaafali ya 39 ya chuo hicho huku akisema hatua hiyo itasaidia kuongeza watenda kazi katika sekta ya anga yenye uhaba mkubwa wa rasilimali watu.

"Nimefarijika kusikia kuwa chuo kikombioni kuanza kutoa mafunzo ya urubani. Mafunzo haya ni muhimu sana kwa taifa letu kwani yatapunguza mzigo kwa serikali na Wazazi wa kugharamia mafunzo haya nje ya nchi ambayo hutolewa kwa gharama kubwa, " alisema.

Alisema serikali imenunua ndege mbili kwa ajili ya mafunzo ya urubani, injini mbili kwa ajili ya mafunzo ya uhandisi wa ndege na 'cabin crew mock ups' kwa ajili ya mafunzo ya wahudumu wa ndani ya ndege.

" Piaserikali imetoa ardhi katika eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) lenye ukubwa wa hekta 60, ambalo litatumika katika kutoa mafunzo ya taaluma za usafiri wa anga. Nimefurahi sana kuona uwekezaji huu mkubwa na muhimu kwa chuo chetu, hivyo, nitoe wito vifaa hivi ambavyo serikali imenunua kwa gharama kubwa, vitunzwe ili Watanzania wengi wanufaike katika kupata mafunzo.

"Napenda kuwapongeza sana nyote kwa jitihada mlizofanya wakati wote wa masomo yenu hadi kufikia hatua hii ya kutunukiwa vyeti leo hii. Hongereni sana. Ninatambua kuwa tuzo mtakayopata leo ni ya msingi kwenu katika safari ndefu ya kuwa wataalam wazuri na mahiri," aliisitiza.

Pia aliwashauri wahitimu hao wasiridhike na ngazi ya taaluma mliyofikia bali waendelee kutafuta maarifa zaidi ili taifa liwe na wataalam wa kutosha na wenye sifa zote zinazohitajika katika sekta ya uchukuzi na usafirishaji.

Kikwete alisema amefarijika kusikia chuo kimeendelea kupanua wigo wa kutoa mafunzo katika sekta ya Uchukuzi, ikiwa ni pamoja na kujiimarisha katika njia zote za usafirishaji yaani usafiri wa anga, majini, reli, barabara na usafiri kwa njia ya mabomba.

Katika hafla hiyo, Kikwete alizindua kitabu ambacho kimeeleza historia ya vhuo tangu kuanzishwa kwake mwaka 1975 hadi sasa. Alisema kitabi hicho kitasaidia kujua chuo kilikotoka, kilipo sasa na kinataka kufika wapi na kwamba kitawezesha kutunza historia ya taasisi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Kaimu Mkuu wa Chuo, Dk. Zainabu Mshana, alisema chuo kimeendelea kuwajengea uwezo wahadhiri na watumishi kwa kuwapeleka masomoni ili kuimarisha kiwango cha maarifa na ujuzi na katika mwaka wa masomo 2023/24, watumishi 71 wako masomoni.

Alisema kati ya hao, 39 wanasoma ngazi ya shahada ya uzamivu (PhD), 24 shahada ya uzamili na mtumishi mmoja anasoma shahada ya kwanza. Pia alisema watumishi watatu wanasoma Mafunzo ya urubani na wanne mafunzo ya leseni za matengenezo ya ndege.

# Bil. 13/- kuendeleza miradi ya Magereza

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema katika mwaka wa fedha wa 2022/23 na 2023/24, serikali imetenga Sh. bilioni 11.15 kwa ajili ya ununuzi wa magari 65 na kuendeleza ujenzi wa majengo ya Magereza kwenye mikoa ya Morogoro, Kigoma, Arusha, Tabora, Dodoma na Pwani.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akifunga mafunzo ya juu na Daraja la Pili kwa Askari wa Magereza katika Chuo cha Mafunzo (TCTA).

Waziri Mkuu alisema serikali imelipatia Jeshi la Magereza magari kwa ajili ya shughuli za utawala na usafirishaji wa mahabusu na hadi kufikia tarehe 22 Mei, 2023 tayari Serikali ilikuwa imeshalipa jumla ya Sh. bilioni 4.459 kwa ajili ya ununuzi wa magari 23 na kati ya hayo, magari 18 ni ya utawala na matano ya mahabusu.

Alisema katika mwaka huu wa fedha, Jeshi la Magereza limetengewa Sh. bilioni 6.691 kwa ajili ya ununuzi wa magari mengine 42 yatakayotumika kwa shughuli za utawala na usafirishaji wa mahabusu.

Pia alisema katika mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetenga Sh. bilioni 2.769 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa magereza ya Gairo na Kilosa mkoani Morogoro, Kakonko mkoani Kigoma, Kaliua na Igunga mkoani Tabora, Karatu mkoani Arusha, Msalato na Isanga Dodoma na Gereza la Kwa Mturuki lililoko Bagamoyo mkoani Pwani.

Alisema miradi hiyo inatekelezwa sambamba na kuanza ujenzi wa magereza mapya ya Kiabakari (Mara), Mpimbwe (Katavi), Sengerema (Mwanza), Kyerwa (Kagera), Kingurungundwa (Lindi) na Mlolo mkoani Iringa.

Waziri Mkuu pia alisema serikali imetenga Sh. milioni 800 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi za Magereza katika mikoa ya Geita, Kigoma, Lindi, Songwe na Tanga pamoja na Sh. milioni 225 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba za maofisa na askari wa Kikosi Maalum cha Kutuliza Ghasia Magerezani, Msalato mkoani Dodoma. "Licha ya hayo, Serikali imetenga shilingi milioni 285 kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama katika magereza matano. Magereza hayo ni Ilagala mkoani Kigoma, Mbarali mkoani Mbeya, Kiteto mkoa wa Manyara, Kingurungundwa mkoani Lindi na Gereza la Kongwa mkoani Dodoma," alisema.

Majaliwa alisema kukamilika kwa miradi hiyo ya ujenzi kutahakikisha uwapo wa huduma bora, mazingira bora ya kazi, makazi bora na mahali salama pa kuhifadhi wafungwa na mahabusu.

Sambamba na kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vitendea kazi, alisema serikali imeendelea kutekeleza mikakati mahsusi ya kuendeleza rasilimali watu, katika mwaka 2021/22 imetoa ajira 1,241 kwa Jeshi la Magereza.

"Katika mwaka 2022/23 imetoa nafasi 734 hawa ni wale walioko mafunzoni. Aidha, katika wa fedha 2023/24 itatoa vibali vya ajira za watumishi 500 ili kupunguza upungufu wa watumishi," alisema.

# Madereva bajaji wagoma madai ya kupinga unyanyasaji

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MADEREVA wa bajaji mjini Morogoro wamegomea kutoa huduma na kuziba barabara ya Masika-Kihonda kwa kupaki vyombo vyao barabarani kwa madai ya kunyanyaswa na mamlaka.

Tukio hilo lilitokea jana na kudumu kwa muda wa saa moja kwa kile kinachodaiwa kuwa ni kunyanyaswa na baadhi ya mamlaka mbalimbali, huku wakidaiwa kuvunja sheria za usalama barabarani.

Mmoja wa madereva wa bajaji, Keneth Matonya, alisema wanaofanya vitendo hivyo ni sekta mbalimbali za barabarani wakiwamo vodafasta, trafiki na wagambo ambao huwakamata mara kwa mara katika maeneo ya mjini wakidaiwa kuwakataza kuingia mjini.

Matonya alisema wanajua wakifanya makosa ya usalama barabarani wanapaswa kukamatwa na askari wa usalama barabarani na sio kikosi cha wagambo au vodafasta ambao hutumia gari kuwafukuza na kuwatishia kuwagonga kitendo kinachotishia usalama wa walio wengi wakihofia kuvunjika miguu.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Morogoro, Gabriel Chiguma, alisema kitendo cha kuziba barabara ni uvunjifu wa amani sababu haki inadaiwa kwa amani na kufuata utaratibu uliopo.

Aliwataka madereva hao wa bajaji kujipanga na madai yao na kuyawasilisha mahali husika kwa kufuata utaratibu bila kuvunja sheria za nchi, kwa sababu kufanya maandamano ni sehemu ya kuvunja sheria.

Chiguma aliwaeleza kuwa serikali kwa kuwapenda iliwashushia kiwango cha adhabu kutoka Sh. 30,000 hadi Sh. 10,000 hivyo kuendelea kulalamika kuwa hawatendewi haki hakutasaidia bali wajipange katika kazi zao na kuzingatia sheria zilizopo.

Mwenyekiti Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Morogoro, Johansen Kakiziba, alisema awali walikubaliana madereva wa bajaji kuacha kutumia njia za katikati ya mji kwa ajili ya kupisha watumiaji wengine wa barabara, lakini kwa sasa yanayofanyika hayaendani na makubaliano.

Alisisitiza kuwa kuna bajaji zaidi ya 3,000 na serikali haiwezi kukamata hovyo, zitazokamatwa ni zile zinazovunja sheria na taratibu za usalama barabarani.



Mkuu wa Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), Mizengo Pinda (katikati), akiwa katika mahafali ya 42 ya chuo hicho yaliyofanyika mjini Songea. Kulia ni Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, na kushoto ni Makamu Mkuu wa OUT, Prof. Elifas Bisanda. **PICHA: MIRAJ MSALA.**

# Wahitimu OUT watakiwa kufanya utafiti kutatua matatizo ya kijamii

**Na Mwandishi Wetu,**
SONGEA

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, amewataka wahitimu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kuitumia elimu waliyoipata kufanya utafiti ili kusaidia kutatua changamoto zinazoikabili jamii inayowazunguka.

Dk. Ndumbaro alitoa rai hiyo juzi wakati wa mahafali ya 42 ya chuo hicho yaliyofanyika katika uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma. Ndumbaro alikuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo.

"Mlichopata hapa si cheti bali ni elimu ambayo ili iwe na manufaa, inabidi mkaitumie kutatua changamoto zilizoko katika jamii kwa kuisaidia na kufanya utafiti wenye tija. Wakati tunaelekea kupata dira mpya ya maendeleo ya taifa ya mwaka 2025, katumieni elimu mliyopata kutoa maoni, uzoefu na maono yenu kupitia mijadala itakayowezesha kupata dira makini kwa taifa letu.

"Pia mnapaswa kutumia ujuzi na maarifa mliyopata kuwa wabunifu wa kuziona fursa na kuzichangamkia ili kuzalisha ajira kwa vijana na jamii kwa jumla," alisema na kukitaka chuo hicho kutumia upekee wake kueneza na kukuza Kiswahili duniani.

Vilevile, alitoa rai kwa chuo kushirikiana na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kuhakikisha ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni ndani na nje ya nchi unafanikiwa ili kuendana na ajenda mahususi ya taifa ya kukuza, kueneza na kubidhaisha Kiswahili Afrika na duniani kwa jumla.

Akizungumza katika mahafali hiyo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Juma Kipanga, akimwakilisha Waziri wa Wizara hiyo, Prof. Adolf Mkenda, alisema mifumo ya elimu imekuwa ikiimarishwa mara kwa mara ili kuendana na mabadiliko ya kidunia katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, teknolojia na kijamii.

"Mabadiliko haya yanailazimu serikali kufanya mapitio ya sera ya elimu kuanzia ngazi ya msingi ili kuiwezesha nchi kupiga hatua. Tunajua kuwa hili pia ni kipaumbele kwa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na chuo hiki kina jukumu la kubeba dhamana ya haya mabadiliko yanayofanyika kwa kuwa ni wadau muhimu wa mabadiliko hayo.

"Lengo ni kuwa na aina ya elimu itayozalisha wahitimu wenye ujuzi, maarifa na uwezo wa kujitegemea katika kujiajiri na kuajiri wengine," alisema Kipanga. Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Prof. Joseph Kuzilwa, alisema kitendo cha serikali kukipatia chuo fedha za ujenzi maabara saba za sayansi za kikanda nchini, ni ishara tosha kuwa serikali inathamini elimu ya juu hususani inayotolewa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kupitia mifumo ya masafa, mtandao, ana kwa ana na huria.

"Chuo hiki kimekuwa mstari wa mbele katika kusambaza utamaduni wetu kupitia lugha ya Kiswahili, kimeanzisha programu za kufundisha Kiswahili Malawi na sasa kinakamilisha mipango ya kufundisha Kiswahili nchini Namibia. Chuo kinakaribisha ushauri na ushirikiano wa namna yoyote ili kufanikisha kukipeleka Kiswahili sehemu mbalimbali duniani," alisema.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Elifas Bisanda, alisema kitendo cha serikali kuendelea kuchangia maendeleo ya chuo ni kuthamini mchango wake kwa jamii na hivyo kukifanya chuo kiendelee kutimiza wajibu wake wa kutoa elimu kwa wanachuo huku wakiwa wanaendelea na shughuli zao huko walipo.

"Si lazima uache kazi zako uende chuoni, tunatumia zaidi TEHAMA katika ufundishaji na hata ada unalipa kwa kiwango unachotaka wewe mwanafunzi.

Pia, mwanafunzi anaweza kuomba kufanya mitihani wakati wowote, ni mifumo tofauti na vyuo vingine," amesema Prof. Bisanda.

Mahafali hayo yalihudhurisha wahitimu 3,980 katika ngazi za astashahada, stashahada, shahada za kwanza, shahada za umahiri na uzamivu. Asilimia 44 ya wahitimu hao ni wanawake na hiyo ni hatua kubwa katika kuinua uwiano wa kijinsia katika elimu ya juu kulinganishwa na miaka 12 iliyopita ambapo wahitimu wanawake walikuwa hawazidi asilimia 25.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga bado mna nafasi CAF

**WIKI** ijayo tunatarajia kushuhudia michezo miwili ya kimataifa kwa klabu za Tanzania, Simba na Yanga ambazo zitaendeleza kampeni ya kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Timu zote zimeshacheza michezo mitatu katika makundi yao na zimepoteza mchezo mmoja na kutoka sare katika michezo miwili matokeo yaliyozifanya timu hizo kuburuza mkia kwenye makundi yao wakiwa na pointi mbili pekee.

Katika hali ya kawaida unaweza kuona ni kama tayari timu zetu zimekosa nafasi ya kusonga mbele kutokana na matokeo yao waliyoyapata baada ya michezo miwili waliyocheza.

Lakini kimsingi bado Simba na Yanga zina nafasi ya kusonga mbele kama watazichanga vyema karata zao kwenye michezo mitatu iliyobaki.

Katika michezo hiyo timu zote zina michezo miwili nyumbani na mchezo mmoja ugenini ili zisonge mbele ni lazima zipate matokeo mazuri katika michezo hiyo mitatu.

Simba itaanza kucheza na Wydad Casablanca Jumanne kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa na siku inayofuata Yanga watawakaribisha Medeama, ni lazima wapate ushindi kwenye michezo hiyo kama kweli wanataka kusonga mbele.

Tunaamini hakuna kinachoshindikana kwenye mpira, wachezaji lazima watambue wanapaswa kujituma zaidi kwenye mechi hizo tatu zilizobakia ili kuendelea kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya klabu bingwa Afrika.

Hakuna haja ya kukata tamaa, nafasi bado zipo kwa timu zote mbili kama watafanikiwa kupata matokeo mazuri katika mechi zote zilizobakia kwenye makundi yao.

Matokeo hayo yanapaswa kuanza kwenye michezo dhidi ya Wydad na Medeama ambazo zitafufua matumaini ya klabu hizi mbili kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Mechi hizi mbili ni muhimu zaidi kwa sababu zitarejesha matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali lakini pia zitawaweka kwenye mazingira mazuri kuelekea michezo inayofuata mbele.

Bado tunasisitiza Simba na Yanga zina nafasi ya kusonga mbele kwenye michuano hii ya Ligi ya Mabingwa Afrika lakini kama zitafanikiwa kushinda michezo yake iliyobakia kwenye makundi yao.

Kimahesabu Simba na Yanga zikishinda michezo yao miwili zitakuwa na pointi nane huku zikibakisha mchezo mmoja kila timu ambao watacheza ugenini.

Simba mchezo wao wa ugenini ni dhidi ya vinara wa kundi lao, Asec Mimosas ya Ivory Coast wakati Yanga mchezo wao wa ugenini ni dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Michezo hiyo ndiyo itatoa picha kamili ya nani anaungana na nani kwenda hatua ya robo fainali na timu gani itaondolewa kwenye michuano hiyo.

Tunazishauri Simba na Yanga, nafasi bado wanazo, lakini ni lazima kuhakikisha michezo hiyo mitatu iliyobakia wanafanya vizuri kwa kupata ushindi

Tunazikumbusha klabu zetu hizi kuwa katika michuano hii ya Klabu Bingwa Afrika kila unapozidi kusonga mbele ndivyo unavyojikusanyia pesa nyingi zaidi.

Kila la heri kwa klabu zetu hizi zinazoipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya vilabu barani Afrika, kufanya vizuri kwa Simba na Yanga kutaendelea kuitangaza Tanzania katika soka la kimataifa lakini pia klabu zenyewe zitajikusanyia pesa nyingi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:**
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Timu ziwe makini, usajili dirisha dogo siyo wa mbwembwe wala siasa

Na Adam Fungamwango

**JANA** saa sita usiku, dirisha la usajili kwa wachezaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, 'first league' na Ligi ya soka Wanawake lilifunguliwa ambapo sasa timu zote hizo zina ruhusa ya kufanya uhamisho kihalali kwa wachezaji wa ndani na nje ya nchi.

Siku chache tu kabla ya kufunguliwa kwa dirisha hili tumeanza kusikia na kuona pilika pilika za klabu mbalimbali, hii ikimtaka huyu na ile ikamtaka mwingine.

Binafsi sipingi pilikapilika hizo, kwa sababu ndiyo usajili wenyewe, mashabiki wa soka duniani kote wanapenda sana mbwembwe kwenye usajili hasa pale wanaposikia klabu wanayoipenda inataka kumchukua mchezaji fulani.

Hata hivyo, kwa upande wa klabu za Tanzania ambazo zinatumia pesa nyingi zinazotoka mifukoni mwa watu kwenye usajili, basi ziwe na nidhamu kwenye hilo.

Binafsi ningependa zisajili wachezaji ambao watakuja kuingia moja kwa moja kwenye timu na siyo wale wa kusubiri eti wazoee ligi au mfumo.

Hiki siyo kipindi cha dirisha kubwa, ni kipindi ambacho klabu yoyote inayojitambua itasajili wachezaji wachache tu, wenye uwezo wa kwenda kuziba mapungufu yaliyopo. Wala siyo kipindi cha kusajili wachezaji kuanzia 10 kwenda mbele na wala siyo kusajili chipukizi.

Ni kipindi cha kusajili wachezaji ambao wameshaiva, wamekomaa na wanakwenda moja kwa moja kufanya kazi.

Kingine ni kuzitahadharisha klabu za Simba na Yanga ambazo zinacheza mechi za kimataifa, hususani Ligi ya Mabingwa Afrika. Ninachoshangaa ni kuona baadhi ya majina ambayo wanataka kuwasajili ni wale ambao timu zao tayari zipo kwenye ligi hiyo hiyo.

Nilidhani kwa timu kama za Simba na Yanga zingesajili wachezaji ambao hawajacheza michuano hiyo ili waje kuwasaidia katika mechi za raundi ya tano na ya sita ambazo zinaweza kuwa muhimu ili kujua hatma yao kwenye mechi za kimataifa.

Katika hali ya kushangaza unaweza kukuta hata viongozi wenyewe wa klabu hawajui hili, kwa sababu tulishawahi kuona Simba ikimsajili Perfect Chikwende kutoka FC Platinum ya Zimbambwe wakidhani kuwa anaweza kucheza Ligi ya Mabingwa, lakini haikuwa hivyo.

Ninavyoziona timu za Simba na Yanga zina mapungufu kwenye vikosi vyao, hivyo wanatakiwa kuongeza wachezaji ambao watakwenda kuwasukuma kwenye michuano hiyo.

Lakini tetesi kuwa wanataka kusajili wachezaji kutoka Jwaneng Galaxy ya Botwana, Medeama ya Ghana, Asec Mimosas ya Ivory Coast na hata Power Dynamos ya Zambia ni kama vile wanasajili tu hao wachezaji kwa ajili ya kuwatumia kwenye ligi ya ndani.

Wachezaji ambao wanatakiwa na klabu hizi kutoka timu hizo walitakiwa wasajiliwe utakapomalizika msimu huu kwa ajili ya kuanza kutumikia msimu ujao tangu mwazo.

Kwa sasa nadhani Simba na Yanga zingetafuta wachezaji wazuri kutoka kwenye klabu ambazo hazijacheza michuano hii inayosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika, mfano kutoka mataifa ya nje ya Afrika, au hata kama barani humu lakini wametoka kwenye timu ambazo hazijacheza Ligi ya Mabingwa wala Shirikisho na hizo ni zile zilizomaliza kuanzia nafasi ya tano kwenye ligi zao.

Wapo wachezaji wazuri tu ambao timu zetu zinaweza kuwasajili kutoka huko.

Mfano mzuri nimesikia Simba ikitaka kumsajili kiungo mkabaji raia wa Chad, Erick Mbangossoum kwani huyu anaichezea klabu ya Union Touarga yenye maskani yake Rabat nchini Morocco.

Huyu moja kwa moja anaweza kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, kwani timu yake haikushiriki michuano yoyote inayosimamiwa na (CAF), kwa sababu timu yake ilimaliza nafasi ya nane kwenye ligi yao.

Kwa upande wa Yanga mchezaji Bonaventure Bonito wa Tengueth ya Senegal, anaweza kuwa na msaada kwa sababu timu yake haijashiriki michuano yoyote ya kimataifa msimu huu.

Kwa klabu ambazo hazichezi mechi za kimataifa, narudia kusema kuwa zisajili wachezaji ambao watafika kwenye kikosi na kucheza moja kwa moja, siyo kusubiri kuzoea mazingira, au ile kauli ya 'tumpe muda.'

## Samia mgeni rasmi tuzo mzalishaji bora

**Na Joseph Mwendapole**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye Tuzo za Rais za Mzalishaji Bora (PMAYA), zinazotarajiwa kufanyika kesho.

Tuzo hizo zimekuwa zikiandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Nchini (CTI) na kuwashirikisha wenye viwanda mbalimbali nchini ambao hushindana kwa kutumia vigezo mbalimbali vilivyowekwa.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodegar Tenga, wakati akizungumza kuhusu tuzo hizo huku akibainisha kuwa tukio hilo la kila mwaka litawashirikisha viongozi mbalimbali wa serikali, wafanyabiashara wakubwa na wawakilishi wa mashirika mbalimbali ya kimataifa.

"Tunamshukuru sana Rais wetu kwa kukubali kuja kutoa tuzo hizi kwa kweli ametupa heshima kubwa kwasababu pamoja na majukumu mengi aliyonayo amekubali kuwa mgeni rasmi hii ni heshima kubwa kwa CTI na wenye viwanda nchini," alisema Tenga.

Pia alisema tuzo hizo zilizotolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2005 zinalenga kutambua mchango wa wenye viwanda kwenye ukuaji wa uchumi nchini na kuongeza ubora kwenye uzalishaji wa bidhaa.

Alisema washindi hupatikana kutokana na vigezo mbalimbali vilivyowekwa baada ya tathmini kubwa kufanywa na mzabuni aliyepewa kandarasi hiyo ambaye huwatembelea wenye viwanda walioingia kwenye mashindano hayo.

Tuzo hizo, alisema zinalenga kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, kuongeza ushindani kwenye sekta ya viwanda, kuongeza tafiti na maendeleo kwenye sekta ya viwanda nchini.

"Tunawashukuru wafadhili wote kwa msaada wao kwasababu bila wao hizi tuzo haziwezi kufanyika, tunamshukuru sana mfadhili mkuu kwenye tuzo za mwaka huu ambaye ni benki ya NBC," alisema

Tenga aliwataja wafadhili wengine wa tuzo hizo mwaka huu kuwa ni benki ya EXIM, Motison Group, TCC, TBL, STAMICO, Total Energies, Kilimanjaro Cables, Alaf Limited, Bonite Bottlers, SBC, Serengeti Breweries Mati Super Brand na Elsewedy Electric East Africa.

Alisema tuzo hizo zimesaidia kwa kiwango kikubwa kwa wenye viwanda kuendelea kuboresha bidhaa wanazozalisha na aliwataka wahakikishe wanazalisha bidhaa ambazo zitashindana kwenye soko la ndani na kwenye masoko ya kimataifa.

"Ili Tanzania ifikie ndoto yake ya kuwa taifa la viwanda lazima wenye viwanda wazalishe kwa wingi na bidhaa ziwe bora kiasi cha kushindana kwenye masoko ya kimataifa tupate fedha za kigeni," alisema Tenga.

# Zanzibar yaipa kongole UNDP ushirikiano miradi ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

ZANZIBAR imelishukuru Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema hayo Ikulu, Zanzibar juzi alipozungumza na Mwakilishi Mkazi wa shirika hilo nchini, Shigeki Komatsubara, aliyefika kumtembelea.

Alisema UNDP imekuwa msaada mkubwa kwa Zanzibar hasa kwa kuendelea kushirikiana nayo katika masuala ya maendeleo ikiwamo kuiongezea nguvu na kuiwezesha kifedha Taasisi ya Ufuatiliaji na Usimamizi Utendaji Kazi Serikalini (PDB) Zanzibar ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Alisema SMZ na UNDP zina ushirikiano wa karibu kwa miaka mingi na wamekuwa wakiunga mkono Serikali kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo.

Rais Dk. Mwinyi alimweleza mgeni wake huyo sera kuu ya uchumi wa Zanzibar ni uchumi wa buluu, hivyo alimweleza kuangalia fursa zaidi za kuunga mkono eneo hilo pamoja na sekta ya utalii.

Dk. Mwinyi pia alipongeza UNDP kwa juhudi zake za kusaidia vyombo vya sheria nchini likiwamo Bunge, Baraza la Wawakilishi na Mahakama kwa kuzijengea uwezo taasisi hizo.

Naye Komatsubara alimwahidi Rais Mwinyi kwamba UNDP itaendeleza ushirikiano kwa kufanya kazi pamoja na SMZ kupitia Uchumi wa Buluu pamoja na kuiunga mkono PDB kupitia miradi mbalimbali ya serikali.

Akizungumza baada ya hafla hiyo, Naibu Ofisa Mtendaji Mkuu wa PDB, Dk. Josephine Rogate Kimaro, alishukuru UNDP kwa ushirikiano mkubwa inaoipatia taasisi yake ikiwamo kuwajengea uwezo kwenye utendaji kazi.

Alisema UNDP imekuwa ikiunga mkono masuala mbalimbali ya maendeleo ya taasisi hiyo hasa kwenye usimamizi na utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kuweka mifumo ya utekeleza wa miradi ya vipaumbele pamoja na kuisaidia taasisi hiyo kwenye ushajihishaji wa rasilimali zake.

UNDP inatekeleza miradi sita barani Afrika ikiwemo mitatu kwa Tanzania na kwa Zanzibar inashirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza miradi ya kupambana na matukio ya uhalifu Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya ufadhili wa serikali ya Uingereza na Umoja wa Ulaya (EU).

Mradi mwingine unaotekelezwa na UNDP ni uwezeshaji kwenye masuala ya utawala wa sheria katika mradi unaoangazia haki na wajibu kwenye masuala ya jinsia hususan wanawake na watoto.



Wahitimu wa Chuo cha wahudumu wa ndege cha Shirika la Ndege (ATCL) wakifurahia wakati wa mahafali yao yaliyofanyika jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wadau wageukia taasisi za kidini mikopo kausha damu

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wa sekta binafsi wamezihimiza taasisi za kifedha zinazoendeshwa na madhehebu mbalimbali ya dini, kuangalia namna ya kusaidia Watanzania kuondokana adha wanayoipitia kutokana na uwapo wa mikopo inayowaingiza kwenye matatizo, maarufu kama 'kausha damu'.

Akizungumza juzi mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi wa kampuni inayojihusisha na usafirishaji wa mizigo, Elias Massawe, wakati wa hafla ya uzinduzi wa tawi jipya la Benki ya Mkombozi, alisema Watanzania wanalia kutokana na mikopo hiyo.

Pia alishauri kuwa ni vizuri benki hiyo ambayo inasimamiwa na Kanisa Katoliki, kuona ni namna gani inawapatia wananchi mikopo rafiki pamoja na elimu ya ujasiriamali itakayowawezesha kujua wanatumiaje fedha walizopatiwa ili ziwaingizie faida na kufanya marejesho kwa wakati.

"Tuanze kuona sasa kwamba hii mikopo kausha damu wananchi wanaepukanaje nayo. benki ifundishe watu kuwa wajasiriamali, wapatiwe wataalamu wa kuwaelekeza kuhusu biashara za kisasa na nina hakika atajua namna ya kuwekeza na kurudisha ndani ya benki," alishauri Massawe

Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Mkombozi, Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya, alisema wale wanaotoa mikopo ya kausha damu hawatoi kwa lengo la kuwasaidia watu.

Alisema watu wanakwenda kwa mtu na kumwambia Sh. 200,000 watalipa 20,000 baada ya mwezi bila kuona kwamba mtu anazitumia kwa lengo gani na bila kumsaidia azitumiaje ili zizae.

"Yule anayetoa anachojali ni faida tu. Kwa hiyo kwa mfano mama anakuja kukopa kwa ajili ya kufanya sherehe ya 'kitchen part' na yule mkopeshaji anampa tu, hamwambii mama unachokikopea si sahihi. Huwezi kukopa fedha ukaenda kufanya 'kitchen part na' utalipaje hilo deni?

"Tatizo kubwa ni elimu kwa mkopaji na hapo ndipo tofauti ya sisi Mkombozi na wakopeshaji wengine. Tunamtazama mtu, tunamwuliza unakopa kwa ajili ya nini na tunamfundisha asije akafanya makosa. Tunamtaka akafanyie kazi kile alichokikopea ambacho kinalipa ili alipe deni lake," alisema.

Askofu Mkuu Kinyaiya aliongeza kuwa mikakati yao mikubwa ni kumsaidia mtu kupata elimu sahihi na kumfuatilia kwa karibu na kwamba maofisa wao wanawafuatilia wakopaji kila wiki kuhakikisha fedha waliyoichukua inazaa na kuwapatia ushauri.

# Majaliwa aagiza kero wamiliki malori zitatuliwe

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Uchukuzi kufanya vikao vya mara kwa mara na Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA) ili kutatua changamoto zinazowakabili ili kuboresha sekta ya usafirishaji.

Amewataka wamiliki wa malori kuwajali madereva wao ikiwamo kuwaboreshea maslahi yao.

Aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipokutana na wadau wa sekta ya usafirishaji waliohudhuria uzinduzi wa kanzidata ya madeveva wa malori nchini iliyoandandaliwa na TATOA.

Katika uzinduzi huo, TATOA imekabidhi Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuwasaidia wananchi waliopata maporomoko ya matope yaliyotokea Katesh, Hanang mkoani Manyara.

Majaliwa alisema watu hao ni muhimu, hivyo kuna haja ya wizara hiyo kukutana nao na kufanya vikao vinne kwa mwaka ili kujua changamoto zao na kuzifanyia kazi.

Pia alisema viongozi wanatambua mchango wao katika kukuza pato la taifa na kusaidia kupunguza tatizo la ajira.

Alisema sekta ya usafirishaji inatoa ajira nyingi katika makundi tofauti na kusaidia kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo serikali itaendelea kushirikiana nao katika kuhakikisha sekta ya usafirishaji inafanya vizuri.

Waziri Mkuu alisema maendeleo walioyafanya ni kuhakikisha wanaweka miundombinu, sera na taratibu za miongozo katika kuboresha sekta hiyo.

Majaliwa alisema serikali imekamilisha ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 2,183.82 na kilomita 14,348 za changarawe na imeendelea na matengenezo ya kawaida ili zipitike.

Majaliwa aliitaka TATOA kuunga mkono bandari ili ziendelee kuwa bora na wafanyabiashara wazifurahie kuzitumia na kuongeza uchumi wa nchi.

Kuhusu uzinduzi wa kanzidata hiyo alisema, TATOA imefanya jambo muhimu ambalo litasaidia ulinzi katika mali zao pamoja na wateja na kusaidia madereva kuacha wingi wa malori njiani bila ya mawasiliano kwa wahusika na sasa kuwa wazi.

Pia aliwataka TATOA kutoa elimu kwa madereva wao ili kufuata sheria za barabarani na kuepusha ajali zinazojitokeza.

"Ni vizuri madereva wa nchini kuongeza umakini barabarani kwa kuzingatia sheria za usalama barabarni ili kupunguza na kuondokana na ajali hasa tunapoelekea sikukuu na mwisho wa mwaka kwa maslahi makubwa ya taifa,"alisema.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, aliwapongeza viongozi wa TATOA kwa ubunifu wao mkubwa wa kuamua kuandaa kanzidata hiyo.

Alisema serikalini kuna mfumo wa kusajili madereva ulioko chini ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ambao umesajili madereva 19,709 wakiwamo wa mabasi na malori.

Mwenyekiti wa TATOA, Elias Lukumay, alisema kuundwa kwa kanzidata hiyo kutasaidia mambo mengi kwa kuwa ni chombo chenye nguvu na kitakuwa na taarifa zaidi ya majina na leseni zao.

Mwakilishi wa Balozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Louis Kisombo, alisema aliomba suala la kuunda kamati ya pamoja ya kufuatilia malalamiko ya madereva lifanyiwe kazi mapema ifikapo Januari, 2024.



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis (kushoto) akipata maelezo ya namna kiungo saidizi kwa mtu aliyekatwa mguu chini ya goti kinavyofanya kazi kutoka kwa Alkado Benedicto (kulia), mtaalamu wa kutengeneza viungo hivyo hospitali ya CCBRT, alipotembelea banda la hospitali hiyo katika maadhimisho ya wiki ya Ustawi wa Jamii na miaka 50 ya Chuo cha Ustawi wa Jamii yanayoendelea katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA:MPIGAPICHA WETU.**

# Kairuki ataka mafunzo yenye hadhi kimataifa

**Na Happiness Shayo**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, amekiagiza Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) kujikita katika kutoa mafunzo yenye weledi, ubora na viwango vya hali ya juu ili kuendana na hadhi ya utoaji huduma kwa watalii kimataifa.

Kairuki aliyasema hayo juzi alipofanya ziara ya kikazi katika chuo hicho kwa lengo la kukagua utekelezaji wa majukumu yake na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazokikabili.

"Tumeendelea kuwasisitiza kuhusiana na dhamana ambayo wamepewa na serikali katika kuandaa wahitimu wenye weledi, ubora na viwango vya hali ya juu ili watakapoenda huko, wakatoe huduma kwenye sekta ya utalii pamoja na maeneo ya uratibu wa matukio inayoakisi taswira ya taifa letu," alisema.

Waziri Kairuki pia alisisitiza suala la kuwaandaa vyema wakufunzi katika masuala ya kitaalamu ya ukarimu, utalii, teknolojia ya Habari na mawasiliano (TEHAMA), kujiamini na kuwa na uwezo wa kumudu lugha zaidi ya moja ili wawe na ushindani katika soko la ajira kitaifa na kimataifa.

Katika hatua nyingine, Kairuki aliitaka menejimenti ya chuo kutafuta fursa mbalimbali na kushirikiana na vyuo vingine vya utalii vya nje ya nchi kama Kenya, Ufaransa, Marekani na Canada ili kuendelea kujifunza kutoka kwao.

Kuhusu miradi ya maendeleo, Kairuki alisema kwa kuwa chuo hicho kina kampasi mbalimbali jijini Arusha, Mwanza na Dar es Salaam, kiangalie namna ya kudahili wanafunzi wengi zaidi na kukidhi kiu ya kupata wataalamu ambao waajiri wangependa kuwapata.

Ziara hiyo ni mwendelezo wa ziara za Waziri Kairuki za kujifunza namna taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii zinavyofanya kazi na kusikiliza na kutatua changamoto zinazozikabili.

# Vijana wapewa vitambulisho askari wanyamapori

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA 32 wa vijiji vya Mlazo na Ndogowe, Kata ya Nghambaku, Chamwino mkoani Dodoma, wamekabidhiwa vitambulisho vya kuwatambua rasmi kuwa ni Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS).

Wamekabidhiwa vitambulisho hivyo baada ya kuhitimu mafunzo katika Chuo cha Uhifadhi wa Wanyamapori Likuyu Sekamaganga kilichoko mkoani Ruvuma.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Chamwino katika hafla fupi ya kukabidhi vitambulisho hivyo, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Neema Nyalege, alisema vitambulisho hivyo vitawapa askari hao nguvu za kisheria za kutekeleza majukumu ya uhifadhi.

Nyalege aliwaasa vijana hao kuzingatia maadili, uadilifu na uzalendo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Pia aliwataka wananchi wengine katika Wilaya ya Chamwino na jijini humo kutenga maeneo ya vijiji vyao kwa lengo la kuanzisha Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori ili kunufaika na matunda yatokanayo na uhifadhi zikiwamo mvua za kutosha na kujiingizia kipato kwa shughuli za utalii.

Kaimu Mkurugenzi wa Wanyamapori kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Kay Kagaruki, alisema kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kupitia mradi wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara kwa ufadhili wa mfuko wa mazingira duniani, iliwezesha ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi kwa kuanzisha mchakato wa kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Chamwino.

Alisema awali mchakato huo ulikusudiwa kushirikisha vijiji 10 vya Tarafa ya Mpwayungu ambapo wataalamu wa wizara pamoja na wilaya walitoa elimu ya umuhimu wa uhifadhi na namna ya kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yao.

"Hadi sasa ni vijiji viwili vya Mlazo na Ndogowe vilivyofanikiwa kuendelea na mchakato huo ambavyo wizara kupitia mradi wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara iliwezesha askari hao 32 kupata mafunzo katika chuo hicho," alisema.

Kagaruki ametoa wito kwa wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, CBO na VGS kuendelea kulinda na kutumia kwa uendelevu rasilimali zinazopatikana katika maeneo yao ili ziweze kutumiwa na vizazi vijavyo.

Pia aliwataka vijana hao kuwa mabalozi wazuri katika uhifadhi ili kuondoa dhana potofu kwa baadhi ya wananchi wanaoamini kutenga eneo la WMA ni kuuza ardhi yao.

Katibu wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Jamii- Chamwino, Godfrey Luguli, aliishukuru wizara pamoja na UNDP kwa kuwapatia elimu iliyowawezesha kuanza mchakato wa kuanzisha Jumuiya hiyo baada ya kutembelea na kujionea namna vijiji vingine vilivyonufaika kupitia mradi huo.

Alisema jambo hilo linawaondolea wananchi adha mbalimbali ikiwa ni pamoja na michango ya maendeleo ya mara kwa mara katika maeneo yao, lakini pia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo yao kutokana na fedha zinazotokana na uhifadhi.



# ‘Wafichueni mabosi wadhalilishaji kazini’

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAFANYAKAZI nchini wametakiwa kutoa taarifa za unyanyasaji wanaofanyiwa na viongozi wao sehemu za kazi ili sheria ichukue mkondo wake na kutokomeza vitendo hivyo.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi, Teknolojia, Habari na Ufundi Stadi (RAAWU), Simon Mbai, alitoa rai hiyo wakati wa mafunzo kwa viongozi wa kamati za wanawake chama hicho Taifa iliyofanyika jijini hapa.

“Najua bado kuna wafanyakazi wanaombwa rushwa ya ngono hasa wanawake, kupitia semina hii mtajengewa uelewa zaidi kuhusu kuzuia hayo yasiendelee kujitokeza kwenye mahali pa kazi,” alisema

Alisema serikali iliruhusu vyama vya wafanyakazi sehemu za kazi ili kutetea haki na maslahi ya wafanyakazi.

Aliwataka wafanyakazi waendelee kushirikiana ili kudumisha usawa wa kijinsia sehemu za kazi.

Mbai, alisema kamati za wanawake zinaonyesha umahiri katika kuibua hoja kuhusiana na maslahi na maendeleo ya wanawake nchini.

Aliwataka kufanyakazi kwa uadilifu ili kuhakikisha wanafikia malengo waliyowekewe na waajiri wao na kuleta ufanisi sehemu za kazi.

Awali Kaimu Mwenyekiti wa Wafanyakazi Wanawake RAAWU, Emmy Chitalika, alisema mafunzo hayo yanawashirikisha viongozi wa kamati hizo kutoka Kanda ya Mashariki, Nyanda za Juu Kusini, Kati, Ziwa na Kaskazini.

Chitalika alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo viongozi hao ili kwenda kuwasaidia wafanyakazi wengine wanawake kwenye kanda zao.

Alisema viongozi hao pia watapatiwa mafunzo ya ujasiriamali ili kuongeza vipato vya familia zao na kujadiliana changamato zinazojitokeza sehemu za kazi.

Mwenyekiti wa RAAWU Tawi la Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana, Dk. Tumaini Sanga, alisema wafanyakazi wanawake wanatakiwa kuacha kutoa rushwa ya ngono ili kupata upendeleo sehemu za kazi.

Dk. Sanga aliwataka wanawake kujiamini kwa sababu wameonyesha uwezo mkubwa na uaminifu katika maeneo wanayofanyakazi.



Waziri wa Fedha Dk Mwigulu Nchemba akikata utepe kwenye ufunguzi wa tawi la PBZ Bank Dodoma uliofanyika jana, kutoka kushoto wa pili ni Naibu Waziri wa Fedha Zanzibar All Suleiman Ameir, watatu ni Mkurugenzi Mtendaji wa PBZ Dk Muhsin Salim Masoud kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bank ya PBZ Dk Esteller Ngoma Hassan. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yawatangazia neema wauzaji dhahabu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeanza mchakato wa kupunguza bei ya mrabaha kwa wauzaji wa dhahabu nchini kutoka asilimia 9.3 hadi 7.3 ili kuwavutia kufanya biashara yao kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Pia, imesema BoT inaendelea na ununuzi wa madini hayo kutoka kwa wauzaji hao kwa kutumia bei ya Soko la Dunia.

Meneja Msaidizi Masoko ya Fedha BoT, Dk. Anna Lyimo, aliyasema hayo juzi wakati akijibu hoja zilizotolewa na wadau wa biashara hiyo na malalamiko ya tozo kubwa ya mrabaha.

“Mchakato wa kupata punguzo la mrabaha kutoka asilimia 9.3 hadi asilimia 7.3 unaendelea na mwafaka utafikiwa... kwa sasa BoT wananunua kwa mrabaha wa asilimia 9.3, tutakaa na wadau kujadiliana ili kupata bei itakayovutia uuzaji wa dhahabu kupitia BoT,” alisema Dk. Lyimo.

Akifungua kikao hicho, Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alisema lengo la Serikali kukutana na wadau hao ni kusikiliza changamoto ya madini hayo kutochangia vizuri katika uchumi wa taifa kupitia fedha za kigeni.

Alisema katika mwaka huu wa fedha wa 2023/24, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kununua dhahabu tani sita.

“Ni dhamira ya BoT kununua dhahabu katika utaratibu uliopo hivyo tuchangamkie fursa hii ili tuchangie kukuza uchumi wa nchi maana Benki Kuu itakuwa soko la kwanza la uhakika la kununua dhahabu kutoka kwa wadau wa biashara ya madini,” alisema Mavunde.

Alisema Serikali ina mfuko wa dhamana ulioanzishwa kwa lengo la kuchochea uchumi kwa wachimbaji kupitia mikopo huku akitoa rai kwa wafanyabiashara walio tayari kuchangamkia fursa hiyo.

Alifafanua kuwa sekta ya madini nchini inachangia ukuaji uchumi na kwamba kwa mwaka 2022/23 imechangia upatikanaji wa fedha za kigeni kwa asilimia 56 ya mauzo ya bidhaa zote nje ya nchi.

“Changamoto ni kwamba takwimu zinaonyesha zaidi ya bidhaa za dola za Marekani bilioni 3.3 ziliuzwa nje ya nchi, lakini hazikuwepo katika uchumi wa kawaida wa nchi, nchi ina changamoto ya upatikanaji wa fedha za kigeni na tulipofuatilia tulibaini sababu kubwa ni wafanyabiashara wengi kukosa mitaji ya kufanya biashara ya madini.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Msafiri Mbibo, alisema katika kikao hicho watajadili kuongeza uzalishaji, kupata mikopo, masoko na mitaji, changamoto za uzalishaji na nini kifanyike.

“Tumeshakubaliana na Tume ya Madini kuorodhesha baadhi ya wachimbaji na wafanyabiashara wenye kukopesheka ili wapewe mikopo, lengo ni kuongeza uzalishaji na mapato ili sekta hiyo izidi kuchangia uchumi wa nchi,” alisema.

# Serikali yakusanya takwimu ajira kielektroniki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetumia Shilingi 346,920,000 kutengeneza mfumo wa kitaifa wa kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za soko la ajira kuanzia ngazi ya wilaya hadi taifa.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi,Vijana, Ajira na wenye ulemavu Patrobas Katambi wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake.

Katambi, alisema mfumo huo utasaidia kudhibiti matapeli kwenye soko la ajira ambao wamekuwa wakitangaza nafasi kazi na kuhitaji malipo.

“Katika soko la ajira za nje ya nchi mfumo huu utasaidia kupunguza shida ya Watanzania kupokonywa pasipoti zao wanapokuwa mataifa ya watu, kunyanyaswa kigono na vitendo vingine vya udhalilishaji,” alisema na kuongeza:

“Mfumo huu utasaidia kuratibu ajira zote za ndani na nje ya nchi kwani hivi sasa unasikia kuna Mtanzania amekufa nje ya nchi, lakini haijulikani amekwendaje huko. ”

Alisema kwa mwaka 2021/22, ajira zilizozalishwa nchini kutokana na uwekezaji wa serikali na sekta binafsi ni 1,226,925.

“Wastani wa ajira 670,140 kutoka miradi ya serikali kuu, serikali za mitaa, mashirika na taasisi za umma na wastani wa ajira 556,785 katika sekta binafsi,” alisema

Alisema serikali imekamilisha maandalizi ya vijana 6,000 watakaoanza mafunzo ya uanagenzi awamu ya sita katika vyuo 42 nchini kuanzia Januari 2024 kwa gharama ya Shilingi 346,920,000.

“Serikali pia imefanya mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi wa hoteli 637 wa Mkoa wa Arusha lengo likiwa ni kuwajengea ujuzi ili kuhudumia wageni wakiwemo watalii kuhakikisha nchi yetu inafikisha watalii milioni tano kwa mwaka na kiasi cha fedha kilichotumika ni Sh. 157,000,000,” alisema Katambi.

Alisema ofisi yake imeendelea kuratibu ajira za wageni na kwamba imepokea maombi 8,392 ya vibali vya kazi na kufanyiwa kazi, kati ya hayo 7,729 yamekubaliwa na 82 kukataliwa kutokana na kutokidhi vigezo vya kisheria.

Kuhusu waajiri wanaokiuka sheria za kazi Katambi, alisema 199 wameonywa na kutakiwa kurekebisha mapungufu ya kisheria na wengine wawili kufikishwa mahakamani.

“Kuhusu huduma za watu wenye ulemavu nchini, serikali imetengeneza mfumo utakaosaidia upatikanaji wa taarifa zao na kurahisisha utoaji huduma kwa kundi hili muhimu nchini,” alisema.





# Othman akoshwa na ufugaji nyuki

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kuna haja ya ufugaji wa nyuki kuwa ajenda ya kitaifa kwa kuwa ni miongoni mwa mazao yenye fursa kiuchumi kwa wananchi kukuza kipato na kupambana na umasikini.

Othman aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Jumuiya ya Wafugaji Nyuki Zanzibar (ZABA) katika eneo la Kitogani Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema kuna haja ya ufugaji na uchakataji wa bidhaa zake kuifanya kuwa ajenda ya kitaifa kwa kutengenezewa mazingira yatakayoleta faida zaidi kwa wananchi na taifa.

Makamu wa Kwana wa Rais alisema kuwapo sera na sheria ya mazao ya nyuki na uchakataji wake ni changamoto ambayo serikali inahitaji kuifanyia kazi ili kuongeza tija kwa wananchi na taifa.

Alisema kinachohitajika ni kujenga mazingira ya kuzalisha asali na mazao mengine yanayotokana na asali ili kuuzwa kwa bei kubwa kama zinavyofanya nchi nyingine duniani.

Serikali, alisema inahitaji kujenga uwelewa zaidi kwa wananchi na watendaji na kulifanya zao hilo la kitaifa kuendelezwa kwa juhudi za pamoja hasa katika uchakataji wa bidhaa na kuleta tija zaidi.

Alisema iwapo wafugaji wa nyuki watazalisha kwa wingi na kwa ubora na kujitangaza katika masoko duniani, asali yao itauzwa kwa bei kubwa kama ilivyo kwa nchi nyingine.

Kwa mujibu wa Othman, Zanzibar ina asili ya kuwa na bidhaa zenye ubora ikiwemo asali inayoweza kuuzwa kwa thamani kubwa iwapo itachakatwa kitaalamu na kutangazwa zaidi katika masoko tafauti.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahamoud, aliwaahidi wanakikundi hao kuwa Serikali itachangia magari nane, kutengeneza eneo la maegesho, pikipiki na tangi la maji ili kuunga mkono umoja huo.

Alisema mkoa huo una misitu mikubwa ya kitaifa miwili na ya jamii ipatayo 25 ambayo iwapo itatumika vyema itakuwa ghala kubwa la asali.

Naibu Katibu wa Umoja huo, Abdu Baruan Abdalla, alisema Serikali imewasaidia kuboresha mazingira ya ufugaji nyuki na uchakataji wa mazao yatokanayo na mdudu huyo kwa faida yao na taifa.



Makamu wa Pili wa Rais Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza katika uzinduzi wa kituo cha mawasiliano ya magonjwa ya milipuko (Zanzibar Afya Call Center) katika Viwanja vya Magomeni visiwani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yajizatiti magonjwa ya milipuko

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) inaendelea kuweka mazingira bora kudhibiti magonjwa ya milipuko visiwani hapa.

Hemed aliyasema hayo jana katika uzinduzi wa kituo cha mawasiliano ya magonjwa ya milipuko uliofanyika Viwanja vya Magomeni, Zanzibar.

Alisema sekta ya afya Zanzibar imechukua hatua katika kuboresha upatikanaji na utoaji wa huduma bora za afya na kudhibiti magonjwa hayo ambayo ni changamoto kutokana na kutokuwa na njia bora za mawasiliano kutoka kwa mwananchi kwenda katika mifumo ya afya.

Alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizokumbwa na janga la Uviko-19 ambalo liliua watu wengi duniani na kuathiri mifumo ya uchumi kutokana na ugumu wa kusambaza taarifa kutoka kwa wananchi kwenda Serikalini juu ya ugonjwa huo.

Hemed alisema uzinduzi wa kituo hicho ni mwarobaini wa upatikanaji wa mawasiliano baina ya wananchi na watoa huduma za afya dhidi ya magonjwa ya milipuko yatakapotokea na kuwataka kukitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ili kurahisisha upatikanaji wa matibabu kwa wakati.

"Kituo hiki kitatoa faida nyingi kwa wananchi ikiwa ni pamoja na mgonjwa kuelekezwa sehemu sahihi ya kupata matibabu kulingana na ugonjwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Wizara ya Afya," alisema.

Hemed alisema kituo hicho kitawasaidia wananchi visiwani hapa, watalii na wageni kufahamu namna ya kujiunga na Mfuko wa wa Huduma za Bima ya Afya Zanzibar, masharti na faida zake.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema uendeshaji wa kituo hicho unahitaji fedha na nyenzo za kutosha ili kifanye kazi kwa ufanisi na weledi wa kuwahudumia Wazanzibari na wageni kwa wakati.

Mazrui aliwataka wahudumu wa kituo hicho kufanya kazi kwa uaminifu, uadilifu na ari ili kuendana na kasi ya SMZ ya kuwatumikia wananchi na kutoa huduma bora za afya kwa wote.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Awety Atie, alisema wataendelea kushirikiana na SMZ kukiendesha kituo hicho ambacho kitafanya kazi kwa mfumo wa kidijitali kwa kipindi cha miaka mitano.

Atie, aliwataka wananchi kukitumia kituo hicho wanapopatwa na dharura, kupata ufafanuzi na ufumbuzi juu ya masuala ya afya kwa kupiga simu bure namba 190 ama kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kupitia namba 30.

# Wizara yajisifu kasi usambazaji maji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar imefanikiwa kusambaza maji safi na salama kwa wananchi visiwani hapa kwa asilimia 67 baada ya kuboresha miundombinu ya maji na nishati, imeelezwa.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Shaibu Hassan Kaduara, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na mikakati na mafanikio ya wizara yake kuelekea Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kaduara alisema wajibu wa wizara yake ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo ili kuwaondolea usumbufu katika baadhi ya maeneo.

Alisema Serikali imejenga tangi la maji lenye ujazo wa mita milioni moja katika maeneo ya Tumbatu ili kuwaondolea usumbufu wakazi wa kisiwa hicho kwa kukosa maji.

Waziri alisema miongoni mwao vipaumbele katika wizara hiyo ni kuendelea kusimamia rasilimali zisizorejesheka ili zisipotee nchini. Hata hivyo, Kaduara alisema uzalishaji wa maji umeongezeka na kufikia asilimia 67 kulingana na ongezeko la watu na kwamba matarajio yao ni kuongeza uzalishaji wa huduma hiyo hadi kufikia asilimia 77 ifikapo mwaka 2025.

Kuhusu umeme, Waziri Kaduara alisema serikali imetiliana saini mkataba na Kampuni ya Energean (ISR) ya Marekani kuzalisha umeme wa jua na kusambaza kwa wananchi.

Alisema sekta ya nishati imefanya ukarabati wa miundombinu ya umeme na kufikia wastani wa megawati 25 hadi megawati 30 ili wananchi waweze kunufaika na huduma hiyo. Aliwataka wananchi ambao hawajafikiwa huduma hiyo kuwa wavumilivu wakati wizara inaendelea na mikakati yake kuhakikisha wananchi wote wanapata.



VANESSA
UKURASA 12



JUMAMOSI DESEMBA 16, 2023



# ITAKUWAJE WAKIWA PAMOJA?

ITAKUWAJE kama ndoto ya mdau mkongwe wa muziki nchini na meneja wa lebo maarufu ya WCB, Mkubwa Fella kama itakuwa kweli?

Ndoto yake ambayo anataka itimie ni kuwaona vijana wake aliowalea tangu wakiwa wadogo Aslay na Mbosso wanakuwa pamoja tena baada ya kutengana kwa miaka mingi.

Ni wazi Fella hajataka kufurahisha watu kwa kufichua ndoto yake hiyo, bali pengine ni maono yake halisi ambayo anayafanyia kazi kila siku.

Wasanii hao wawili walitengana baada ya kundi la Yamoto Band lililoundwa na wasanii wanne kuvunjika katika mazingira ya kutatanisha.

Hata hivyo ndoto hiyo itatimia endapo tu mkakati wa Mkubwa Fella wa kumsainisha Aslay katika lebo ya WCB utafanikiwa.

Hata hivyo mkongwe huyo amefichua kwamba mpango huo uko katika hatua nzuri.

Kama mpango huo utakubalika na mmiliki wa lebo hiyo Diamond Platnumz, basi Mbosso na Aslay watarudi tena kuwa pamoja na hapo ndani ya WCB kutakuwa na wasanii wawili wenye vipaji vya kushangaza.

Wote wawili ni wazuri katika nyimbo za kimahaba, tena sauti zao zinanoga zaidi katika kunung'unikia mapenzi ambazo meneja huyo wa iliyokuwa Yamoto Band huwa anafurahishwa nazo.

Kulingana na Mkubwa Fella, tayari amemfikishia Diamond Platnumz kuhusu mpango huo na kwamba kutokana na roho yake nzuri anatumaini kuukubali.

"Wakati Mbosso aliondoka Yamoto kujiunga na WCB, nilitoa baraka zangu zote na Diamond ndiye alikuwa mstari wa mbele kumpokea. Na ndio sasa hivi nafanya mpango naongea na Naseeb na Mungu akijalia yule Aslay ampe shavu kidogo, ni kijana ana talanta kubwa sana," Alikaririwa akisema Mkubwa Fella.

Hata hivyo, Aslay mwenyewe wakati akizungumza na chombo kimoja cha habari, alikanusha kuwepo kwa uvumi huo, akisema kwamba kwa bahati mbaya sasa amesaini lebo ya Rockstar ya Afrika Kusini na hana mpango wowote wa kuingia Wasafi.

BASI SAWA

## Zabron Singers wafunga 2023 na 'Sisi Ndo Wale'

BAADA ya kutamba na wimbo wa Upo Single, kundi nyota la muziki wa Injili nchini, Zabron Singers limefunga mwaka vizuri kwa kuachia ngoma yao mpya inayoitwa Sisi Ndio Wale.



Kundi hilo kutoka Kahama mkoani Shinyanga limepata umaarufu 2023 kwa kutoa nyimbo zinazopendwa na watu wote huku wakijipatia mialiko mingi ndani na nje ya nchi.

Akizungumza na BT, Mwalimu wa Zabron Singers, Japhet Zabron ameweka wazi kuwa Sisi Ndio Wale, ni wimbo wa mwisho kwa mwaka huu na anaamini utawagusa wengi.

"Wimbo umetoka Ijumaa na tayari tumeanza kuona mrejesho mzuri kutoka kwa mashabiki zetu mtandaoni, ni wimbo ambao umewabariki wengi naamini utafunga mwaka huu na kufungua vyema mwaka ujao," alisema Japhet.

## Wema Sepetu hatimaye kaamua...

MWIGIZAJI mkongwe wa Bongo Muvi, Wema Sepetu hatimaye amefanya uamuzi mzito baada ya kutangaza kwamba mtoto wa mpenzi wake, Whozu sasa ni binti yake.

Hatua hiyo ameichukua baada ya majaribio kadhaa ya kupata mtoto kushindikana. Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Wema ameandika ujumbe ukiambatana na video fupi ikimuonyesha mtoto huyo akicheza.

Katika ujumbe huo amesema anapenda kutamka kwamba mtoto huyo ni kipenzi chake, bila kujali atakuwa binte yake wa kweli na atakuwa naye kila wakati maishani mwake.





## MWACHENI VANESSA AFURAHIE NDOA

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva ambaye kwa sasa ameamua kukaa nje ya jukwaa, Vanessa Mdee, amesisitiza kwamba hawezi kufikiria kurudi tena katika muziki.

Vanessa amesema hayo baada ya baadhi ya mashabiki zake kumuomba afikirie tena uamuzi wake huo kwa sababu kwa kipindi kirefu wamekosa vionjo vyake ambavyo viko tofauti.

Mwimbaji huyo amekuwa nje ya ulingo wa sanaa kwa takribani miaka minne baada ya kuingia kufunga ndoa na msanii wa Marekani mwenye asili ya Nigeria, Rotimi.



## Harmonize kaweka alama Afrika

MJADALA kwa sasa ni jinsi mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize anavyofanya vizuri katika majukwaa ya kimataifa na kuwabwaga wasanii wakubwa barani Afrika.

Wimbo wa msanii huyo 'Single Again' umeingia katika tano bora ya nyimbo zilizofanya vizuri katika mtandao wa Spotify kwa bara la Afrika.

Baadhi ya wadau wa muziki wamempongeza Harmonize kwa kufikia hatua hiyo na kueleza wasijitokeze wasanii wengine na kuanza kumpiga vita, badala yake wampe nguvu katika kutoa nyimbo zingine bora zitakazokuwa na ushindani.



## LINAH, TATIZO NYOTA!

**Na Adam Fungamwango**

WASANII wa watu maarufu hupenda sana kutumia mitandao. Huitumia kwa njia mbalimbali, kibiashara, kuwasiliana, kuelimisha jamii na hata kufikisha ujumbe.

Wiki hii wasanii na watu maarufu wameandika vitu vingi kwenye mitandao yao mbalimbali ya kijamii.

Hata hivyo leo tutaweka hizi chake ambazo wameziposti.

**Maisha magumu-Kajala**

Kajala Masanja kupitia mtandao wake wa instagram, akaandoka maneno yafuatayo

"Maisha magumu hadi raha jamani." Yalikuwa ni maneno ya mwigizaji huko mkongwe wa kike na katika mtandao wake akajibiwa na mwigizaji mwenzake za zamani, Elizabeth Michael aliyetamba kwa jina la Lulu, akaandika. "Acha tu." Ilikuwa ni kumsapoti mwenzake Kajala aliyesema maisha ni magumu, akaongezea na utani kuwa hadi raha.

**RIP Zahara-Lady Jaydee**

Msanii na mwanamuziki Lady Jaydee yeye alionekana kuguswa sana na kifo cha msanii wa Afrika Kusini Bulelwa Mkutukana maarufu kama Zahara, aliyefariki dunia nchini Afrika Kusini hivi majuzi akiwa na miaka 36.

"Asante kwa muziki na sauti, vitabaki kuwa kumbukumbu ya milele mioyoni na masikioni mwetu RIP Zahara," akaandika Lady Jaydee kwenye mtandao wake wa instagram.

**Nawakwaza? Semeni!-Billnas**

Msanii mwimbaji maarufu nchini, Billnas, akajitupia kwenye mtandao wake wa instagram akiwa amepiga pamba zake za uhakika, halafu akaandika maneno haya.

"Kama nawakwaza semeni." Haikupita muda, msanii mwenzake, Marioo akajibu. "Hautukwazi tajiri."

**Sasa nimekuwa Ninja-Idriss Sultan**

Msanii vichekesho, mwigizaji na mshindi wa zamani wa mashindano ya Big Brother Africa, yeye amechapisha maneno yake kwenye mtandao wa instagram kuwa kwa anataka kupambana ili angalau apate gari ndogo ya kutembelea maana nauli zimepanda.

"Ni wakati sasa nipambane nipate hata kagari kadogodogo maana nauli zimekuwa kama tunapanda ndege.

Hamuwezi kunijua nikiwa kwenye basi sababu huwa nakaa kininja."

**Tatizo nyota?-Linah**

Linah Sanga, kama kawaida yake, akaposti picha yake akiwa ametupia vitu vyake, amependeza sana. Lakini akaposti maneno hafuatayo.

"Mbona mimi ni mrembo tu jamani?Kwani tatizo nini? Au nyota?" Analalamika mtoto wa watu.

FILAMU

## Issa: Ukipenda boga, penda na ua

**Na Adam Fungamwango**

UKIPENDA ua penda na boga lake. Ni msemo wa kiswahili wenye maana kuwa unapompenda mtu yeyote, basi wapende wa wanaomzunguka, au anaowapenda yeye.

Yeyote anayewapenda watu ambao wanapendwa na anayempenda, anakuwa kwenye wakati mzuri zaidi wa yeye kupendwa zaidi.

Lakini unapowachukia watu wanaomzunguka unayempenda unajiweka kwenye mazingira ya kuchukiwa baadaye.

Hapa tunaiangalia filamu ya 'Issa', inayomzungumzia jamaa mmoja ambaye yeye baada ya kuoa, mtu pekee anayemthamini ni mkewe tu na si mwingine.

Imechezwa na wasanii kama Nasra Juma, Aldin Hilal, Fumo Said, Moud Abdallah, Zainabu Simba, Mariam Bahati, na wengineo.

Issa baada ya kuoa, anamchukua mkewe na kuishi naye huku akiwa hataki ndugu upande wa ukweni nyumbani kwake.

Baba mkwe anaumwa na anakuja mjini kwa ajili ya matibabu hivyo ilibidi afikie kwa binti yake.

Ile kufika tu, anaulizwa atakaa muda gani na Issa anaonekana hakubaliani sana na hilo.

Anakwenda kufuata ushauri wa rafiki yake, naye anamwambia, tatizo la mkwewe ni lake, na baba ya mkewe ni kama baba yake tu.

Anaupuuza ushauri huyo, anarejea nyumbani na kumwambia mkewe hana pesa ya kumlisha na hata ya kuongezea matibabu, hivyo ajiandae kuondoka.

Baba yake kwa kuona mkwewe ni mtata, akaamua kukusanya virago vyake na kuondoka.


Cha ajabu ni kwamba hata alipokuwa anaondoka, begi na mfuko wake ukasachika, eti asije kuiba kitu ndani.Akasachika mpaka mifuko ya shati na suruali.

Mzee anafariki baada ya kufika kijijini. Huku nyuma, Issa anamnyang'anya simu mkewe ili asiwasiliane na ndugu zake.

Hata msiba wa baba yake anakuja kuambiwa na watu baki. Mumewe anamtaza kwenda kuzika. Hata hivyo majirani anamchangia pesa za rambirambi anazozitumia kwa nauli kwenda kuzika baba yake.

Baada ya hapo hakutaka kurejea tena. Habari zikaja kuwa mumewe amepatwa na maradhi ya kupooza. Mke hakutaka kujishughulisha tena, akisema hamtaki tena mwanaume ambaye alimtesa na kuidhalilisha familia yake kiasi cha kusababisha kifo cha baba yake.







# Binti wa Kanye kama baba yake

BINTI mkubwa wa rapa maarufu wa Marekani, Kanye West, ameingia rasmi katika muziki anaofanya baba yake na hivi majuzi amezindua jina lake litakalomtambulisha.

Noth mwenye umri wa miaka 10 ambaye mama yake ni Kim Kardashian, alijitambulisha wakati wa uzinduzi wa albamu ya pamoja na babaake.

Wimbo unaoitwa "You Don't Want" ni miongoni mwa vibao aliohusika kuimba, nyimbo nyingine ni "I love it here, We're gonna take over another year , It's your beste Miss na Miss Westie.



## Oprah anatumia dawa kupunguza mwili

MWENDESHA kipindi cha mazungumzo kutoka Marekani, Oprah Winfrey amesema mwonekano wake mpya unatokana na kuanza kutumia dawa ya kupunguza uzito.

Akiongea na jarida la  People katika mahojiano mapya, tajiri huyo wa vyombo vya habari amesema kwa sasa haoni aibu kutumia dawa hizo kwa kuwa imempatia mwonekano mzuri.

"Sina aibu kabisa kutoka mbele ya  watu wengine, ukweli ni kwamba kuna dawa iliyoidhinishwa kitabibu kwa ajili ya kudhibiti uzito na kuwa na afya bora, nahisi nina nafuu kama nimekombolewa," amesema.

## Meghan atoa kinyongo

RAPA wa Marekani Meghan Thee Stallion, ameendeleza ugomvi na mpenzi wake wa zamani Pardi akisema kamwe hakuweza kudanganya katika maisha yao.

Pardi, alimtuhumu Meghan kwamba amekuwa muongo katika mapenzi yao na kwamba hakuwahi kufurahia mpaka wanaachana.

"Kama unasema sikuzungumza na wewe, basi sikuwa nazungumza na wewe, ulitaka kutafuta sababu ya kunichafua, madai yote yanaonekana kuwa ya kimkakati. Kama siongei kuhusu wewe, kwa nini unanizungumzia? amehoji Meghan.

Mvutano wao ulianza baada ya Meghan kutoa wimbo ambao ndani yake kuna mstari ukimuongelea vibaya Pardi ambaye pia alijibu kwa kuachia wimbo uliomlenga Meghan.





## Jada akumbuka kofi la huba

JADA Smith ambaye ni mwigizaji Will Smith, amefichua kwamba kofi ambalo mumewe alimpiga Chris Rock wakati wa tuzo za Grammy liliokoa ndoa yao.

Katika mahojiano na Daily Mail, Jada amesema kuwa tukio hilo lilikuwa la kushangaza  maishani mwake na kumfanya atambue kuwa yeye na Smith hawataachana.

"Baada ya miaka yote ya kujaribu kufikiria ikiwa ningeondoka kwa Will, lile kofi lilifanya kila kitu kubadilika na kamwe sitamuacha mume wangu," amesema.

## Sheggz kapenda kweli

MTANGAZAJI wa vipindi vya burudani kutoka Nigeria, Sheggz, amemtetea mpenzi wake mwanamuziki Bella Okagbuem akimuelezea ni mtu mwaminifu tofauti anavyoonekana na watu wengine.

Sheggz alitumia ukurasa wake wa X, akielezea kukerwa kwake na matamshi ya aibu na dharau anayotupiwa mke wake na kusisitiza kuwa tabia kama hiyo haikubaliki.

"Mwanamke wangu ni halisi na mwaminifu kwangu," ameandika Sheggz.





# Viongozi wapigwa msasa Sensa 2022

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Loy Ole Sabaya amesema matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 yatawasaidia viongozi na wataalamu kwa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo.

Sabaya aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa mafunzo ya usambazaji na matumizi ya matokeo ya sensa hiyo kwa viongozi wa serikali na makundi maalumu mkoani hapa.

Alisema licha ya kuwa sensa ni muhimu kwa Taifa, matumizi sahihi ya takwimu za matokeo hayo ni muhimu zaidi kwa ajili ya mipango ya maendeleo nchini.

Kwa mujibu wa Sabaya, wao kama viongozi wa CCM, matokeo hayo yana umuhimu katika kupanga mipango ya maendeleo, kufanya ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa Ilani ya chama hicho kwa Arusha na Taifa.

"Sisi kama viongozi ambao ni wawakilishi wa wananchi, tuko tayari kupokea mafunzo haya kwa kuwa yatakuwa na umuhimu kwetu na nchi yetu tunaamini yatatusaidia kwa mkoa na wilaya zetu na Taifa, " alisema wakati akizungumza katika mkutano huo ambao ulikuwa ni wa kwanza tangu achaguliwe kushika nafasi hiyo.

Alitumia fursa hiyo kuwashukuru wajumbe kwa kumchagua na kumpa dhamana ya kuwahudumia wakazi wa Arusha na kuahidi kufanya kazi kwa uadilifu.

Akifungua mkutano huo, Katibu Tawala Msaidizi Utumishi na Rasilimali Watu wa Mkoa huo, David Lyamongi, alisema lengo ni kuyajengea uwezo makundi ya kijamii ya matumizi sahihi ya matokeo ya sensa hiyo ya watu na makazi.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Mkoa wa Arusha, Zaituni Swai, alisema matokeo ya sensa hiyo yalikuwa ni ya kisayansi zaidi licha ya kuonyesha idadi ya Watanzania ni milioni 61, kati ya hao kwa Mkoa wa Arusha wako 2, 356, 255.

"Kupitia matokeo hayo, viongozi na waatalamu wa Mkoa wa Arusha itawawezesha kupanga mipango, itakayokwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050, ambayo ilizinduliwa na Rais wetu (Samia Suluhu Hassan)," alisema.

Waliopatiwa mafunzo hayo ni pamoja na viongozi wa siasa, dini na mila, watendaji wa mkoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, watendaji wa kata, kamati ya sensa mkoa na wawakilishi wa makundi ya kijamii na watu wenye mahitaji maalumu.

# Mchengerwa awabana waganga wakuu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amewataka waganga wakuu wa mikoa na wilaya mkoani hapa na Manyara kutoka ofisini na kwenda kuwahudumia wananchi.

Waziri Mchengerwa alitoa kauli hiyo baada ya kukabidhi magari 13 kwa ajili ya usimamizi shirikishi wa afya kwa mikoa hiyo, Arusha (matano) na Manyara (manane) katika hafla iliyofanyika kwenye viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Mkoa Arusha.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa magari haya kwa ajili ya kusimamia utoaji wa huduma za afya kuanzia ngazi za vijiji hadi mkoa. Kwa sababu hii waganga wakuu wa mikoa na waganga wakuu wa wilaya tokeni ofisini nendeni kufuatilia hali ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

"Pia Rais wetu ameleta vifaa tiba, dawa na sasa ametupatia usafiri huu kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wetu sasa kwa nini wewe usifanye kazi nendeni mkahudumie wananchi," alisema.

Mchengerwa alionya kuwa waganga wakuu watakaoshindwa kutimiza wajibu wao ofisi yake haitasita kuwachukulia hatua za kinidhamu sambamba na madaktari na mauguzi watakaothibika kusababisha vifo vya mama na mtoto kwa uzembe.

Vilevile aliwaagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi nchini kukamilisha ujenzi wa miradi ya maendeleo baada ya serikali kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji, lasivyo watachukuliwa hatua na kuvuliwa nyadhifa.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Dk. Wilson Mahera, alitumia fursa hiyo kutangaza kiama kwa watumishi wa afya ambao wanaofanya uzembe na wenzao wanaowatetea ili wasichukuliwe hatua.

"Kuna watumishi wa afya ambao wenzao wakichukuliwa hatua za kinidhamu kutokana na uzembe katika maeneo ya kazi ikiwemo kusababisha vifo vya mama na mtoto wanaanza kuwatetea. Nataka niwaambie na wao tutawasimamisha kazi," alisema.

Aliwataka waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha magari hayo yanatumika kwa malengo yaliyokusudiwa vinginevyo watachukuliwa hatua. Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, aliishukuru serikali kwa kuwapatia magari hayo kwa ajili ya kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa moja ya magari hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, Juma Hokororo, alisema yatawasaidia kupata taarifa za wagonjwa, dawa na mienendo ya watoa huduma kwa wagonjwa.



Mtaalamu wa Samaki kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Prisca Issangya kushoto akikabidhi baadhi ya vifaa vya kisasa vya Ulinzi Shirikishi wa Bahari kwa Kaimu Mkurugenzi wa Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Merisia Mpalazo kulia, juzi wilayani Mkinga. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# Mongela ajitosa mgogoro wa wananchi, hifadhi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, ametoa siku 10 kwa uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara kufanya tathimini ya mipaka na kutatua mgogoro baina ya hifadhi hiyo na wakazi wa Kijiji cha Buger kilichopo wilayani Karatu mkoani Manyara.

Mongela alitoa agizo hilo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji hicho wakati wa kujadili jinsi ya kutatua mgogoro huo uliodumu kwa zaidi ya miaka nane.

"Hifadhi ni yetu wote, mimi mkuu wa mkoa nina maslahi kwenye hii hifadhi, pia wewe mwananchi una maslahi nayo, sasa kwa kuwa wote tuna maslahi na kitu hiki ni lazima tuwe na uchungu nacho," alisema na kusisitiza:

"Katika jambo hili unapotafuta mwafaka wake, mhifadhi ni lazima tukubaliane kwenye mipaka na nyumba hizi tunaziacha, hivyo natoa wiki moja tuje tupitie mpaka kwa kuangalia ni sehemu gani tunaweza kuwaachia wananchi na sehemu gani ni lazima ibakie hifadhini."

Mongela, alisema baada ya kufanya mapitio ya mipaka, wanatakiwa kupeleka ramani isiyokuwa na mkanganyiko kwa ajili ya kutatuta mgogoro kati ya kijiji na hifadhi.

"Desemba 22 mwaka huu, nitarudi hapa Buger sasa ninaomba tupate watu watatu wenye hekima kubwa ambao wanaweza kukaa kwenye mazingira magumu, wakafikiri na kusaidia kwa kuwa watafanya kazi na timu ya wataalamu wangu kwa ajili ya kutengeneza mpaka wa kudumu na waelewane," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Dadi Kolimba, alisema mgogoro wa mpaka kati ya kijiji hicho na hifadhi hiyo ulianza tangu mwaka 2015 na kwamba Februari 24 , mwaka huu, walifanya mkutano katika kijiji kujadili jinsi ya kutatua mgogoro huo. Mkazi wa Karatu, Emmanuel Matay, alimpongeza Mongela kwa hekima anayotumia kutatua mgogoro huo.

"Mkuu wa Mkoa wewe unafaha kuwa mzee wa mkoa kwa kuwa una uwezo wa kutatua mgogoro huu pasipo kukwaruzana na wananchi kwa kuwa hifadhi ni ya wananchi na inatusaidia miaka yote," alisema.

Mkuu wa Hifadhi hiyo, Eva Malya, alisema baada ya wananchi kuona msitu unakwisha kutokana na uharibifu unaofanyika waliomba ulindwe na Serikali ikachukua uamuzi wa kupandisha hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa kupitia Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara na kuanza kulinda msitu.

Aidha alisema wakati wa kutafsiri mpaka kijiji hicho kwa tangazo la serikali mwaka 2009 ardhini ilionekana msitu ulimegwa na maeneo mengi hayana misitu baada ya kugeuka mashamba na kujengwa nyumba.

" Kwa kuangalia mpaka wa kijiji bado kuna maeneo mengi kuna mashamba ambayo ni zaidi ekari 519 na nyumba za kaya 175, " alisema.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Bibi harusi wa zamani kilio, wa leo shangwe 'mtanikoma!'

**Na Adam Fungamwango**



Harusi za kisasa

KWELI waswahili wanasema kila zama na kitabu chake. Ukiangalia picha, video za harusi au ukiwa kabisa ndani ya ukumbi utaona jinsi mambo yanavyoendelea ambapo unaweza ukadhani ni ya kawaida kama ni mtu wa kizazi hiki.

Wale wazee na ambao kwa sasa ni watu wazima watakumbuka harusi za zamani jinsi zilivyokuwa.

Kwanza kabisa bibi harusi siku ya kuolewa analia unaweza ukadhani anataka kwenda kuchinjwa.

Na asipolia inakuwa kama ni ajabu kubwa, ana anaweza kuwa kama amewatia aibu wazazi na ukoo wake wake.

Na harusi ikiisha ndiyo anakuwa simulizi kubwa, kwani tayari atakuwa amewapa la kusema watu mitaani.

"Yaani bi harusi anaolewa macho makavu kama dagaa kauzu. Yaani ametutia aibu kweli wanawake mwenzake, sijui ana matatizo gani?" Watateta mitaani.

Bi harusi wa zamani hawakuwa wanaonekana hata sura. Ukifanya masihara bwana harusi unaweza hata kubambikiwa mwanamke mwingine siyo uliyemchagua halafu utakuja kushtuka kesho asubuhi.

Ni kwa sababu tu zamani watu walikuwa na maadili, lakini kama ingekuwa hivi sasa wanaume wangeweza kubambikiwa wake wengine tofauti na waliowachagua.

Wapiga picha wenyewe zamani walipata shida sana kupata sura za mabiharusi, na hata akipata basi atakuwa amelia vya kutosha, uso umesawijika, au amenuna.

Yeyote atakayeonekana anatabasamu, basi waswahili wana msemo wao kuwa 'ataimbwa ngomani.'

Yeyote aliyeolewa miaka ya nyuma, mpaka ile ya mwishoni mwa miaka ya 1990, atakwambia jinsi alivyokuwa hana raha siku yake ya harusi, tofauti na wanawake wanaoolewa sasa.

Tunakuja sasa kwa hawa wa kizazi kipya. Eee bwana we, wanakuwa na furaha iliyopitiliza.

Wanafurahi na kucheza wakati mwingine kwa kiwango cha kupitiliza kuliko waalikwa na madansa walioalikwa kwa kazi hiyo.

Bi harusi anaweza akashinda kabisa madansa kwa kucheza siku hiyo. Anacharuka kwa furaha kuliko hata mashoga zake waliokuja kumpa sapoti.

Anakuwa amejipamba kuliko kawaida na hana aibu kabisa ukumbini kama wale bibi na mama zetu.



Harusi za kizamani

Anaingia ukumbini akiwa amechagua kabisa na wimbo wa kuingilia, ambao mara nyingi unakuwa ni wa vijembe kwa wale ambao labda walidhani haolewi.

Watu wanaweza kushangaa kwa nini anachelewa kuingia kumbe, DJ bado hajaupata wimbo ule aliouomba ili aingie ukiwa unapigwa na atacheza kama hana akili nzuri.

"Mtanikoma mwaka huu, mlijifanya nyinyi mna maadili, sijui mmejitulize, mimi mcharuko sitoolewa, haya kiko wapi, nimeolewa sijaolewa?" Ni kijembe kinachopatikana kwenye wimbo au kwa bi harusi mwenyewe.

Wakati mabiharusi wa za zamani wakijiziba hadi nyuso zao, nguo zao au shela hazikuonyesha mwili, pia zilikuwa ndefu mno.

Kwa sasa shela iwe ndefu au fupi, lakini sehemu kubwa ya mwili inaonekana na wakati mwingine mabega yote yanakuwa nje.

Fikiria, kama bi harusi analia, ananuna, anakuwa na majonzi muda wote wa harusi na hata sura yake haonekani vema, anaweza kuongea kweli?

Mabiharusi wa sasa nao wana kipande chao cha risala, ambacho atawashukuru wote, na hata kuelezea jinsi alivyokutana na bwana harusi na wapi.

Mada niliiweka kwenye mtandao na baadhi ya watu wanazoona kwa nini kuna mabadiliko hayo kwa mabiharusi wa zamani na wa sasa haya ndiyo mawazo yao.

"Wanawake wa zamani walikuwa wanaolewa na watu wasiowafahamu ndiyo kwanza wanawaona kwa mara ya kwanza. Na pili baada ya kuolewa walikuwa wanapelekewa mbali sana na kwao kwa hiyo kuonana ni majaliwa tena. Vile vile ukumbukwe wakati huo hakuna teknolojia kama sasa, anaolewa Tabora anakwepekwa Mtwara, hakuna simu wala mitandao ya kijamii, lazima alie, wa sasa hata apelekwe wapi, atapiga simu au kuwasiliana na ndugu mitandaoni," alindika mdau mmoja, mwingine akaandika haya.

"Wanawake wa sasa lazima awe makini kupepesa macho huku na huko ili awalingishie wabaya wake waliokuwa wanasema haolewi, je wapo na wamemuona?"

Yupo aliyeandika kuwa wanaoana wengi wa sasa wanakuwa wameshaanza mapenzi yao kitambo tu, tofauti na zamani walliokuwa wanaoana watu ambao hawafahamiani tabia, wala walikotoka.

"Mimi nadhani kilio kilikuwa kinaletwa na majonzi ya kuiacha familia na kwenda kwa mume. Siku hizi mabibi harusi wanakuwa na furaha kwa sababu kuolewa sio kitu rahisi zama hizi," anaandika mdau mwingine na binti mmoja aliyeolewa karibuni akaandika.

"Sasa hivi tushachoka na maisha, ndoa zenyewe mpaka uenfe Bagamoyo, mara sumbawanga mpaka ukifikishwa Kanisani upo hoi inabidi tu ucheke na kufurahi."

Mmoja yeye akandika maneno haya. "Si unajua mambo ya 'make ups', kope, ukilia unaharibu sura na picha yenyewe ya video."

Wa mwisho akamalizia hivi. "Wachezaji wafurahie jamani, siku hizi siyo mchezo, tumeona stori nyingi unakuta bibi harusi anatangulia ukumbuni halafu mshkaji hatokei, siyo kitu cha kuchukulia poa."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HABARI KIMATAIFA

## Hungary yakasirishwa Ukraine kupewa uanachama EU

**BRUSSELS,** UBELGIJI

NCHI ya Hungary imezuia msaada unaogharimu kiasi cha dola bilioni 55 wa Umoja wa Ulaya (EU) kwa ajili ya Ukraine baada ya kufikiwa makubaliano ya kuanza mazungumzo ya kukubali kujiunga na umoja huo.

Waziri Mkuu wa Hungary, Viktor Orban alipinga kutoa msaada zaidi wa kifedha kwa Ukraine, baada ya kukubaliwa kuanza mazungumzo juu ya kuzipa uanachama wa Umoja wa Ulaya nchi za Ukraine na Moldova.

Viongozi wa umoja huo walisema mazungumzo hayo ya msaada wa ziada kwa Ukraine yatafanyika tena mapema mwaka ujao.

Ukraine inategemea ufadhili kutoka Umoja wa Ulaya na Marekani wakati inapoendelea na mapambano yake dhidi ya vikosi vya Russia.

Hungary ambayo ina uhusiano wa karibu na Russia kwa muda mrefu imepinga uanachama wa Ukraine ndani ya umoja huo.

**DW**

## Ecowas yaisimamisha rasmi Niger

**ABUJA,** NIGERIA

JUMUIYA ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (Ecowas) imesimamisha rasmi uanachama wa nchi ya Niger baada ya serikali ya kijeshi kukataa kumrejesha madarakani rais aliyeondolewa madarakani Mohamed Bazoum.

Bazoum alipinduliwa katika mapinduzi ya kijeshi mwezi Julai mwaka huu.

Ecowas ilisema katika taarifa yake iliyotolewa Alhamisi kwamba mkutano wa viongozi nchi wanachama uliofanyika Nigeria ulitambua serikali ya Rais Bazoum ilipinduliwa kikamilifu katika mapinduzi hayo ya kijeshi.

Niger imesimamishwa katika vyombo vya kufanya maamuzi vya Ecowas hadi utaratibu wa kikatiba utakapo rejeshwa nchini humo.

Awali Ecowas ilichukulia kama jaribio la mapinduzi, na hivyo kusababisha kuchelewa kusimamisha uanachama wa nchi hiyo.

Ecowas iliweka vikwazo na hata kutishia kuingilia kijeshi baada ya mapinduzi.

**BBC**

# Marekani yazidi kuibana Israel isitishe kuishambulia Gaza

**TEL AVIV,** ISRAEL

VIONGOZI mbalimbali duniani wameendelea kutoa wito wa kusitishwa kwa vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza kati ya vikosi vya Israel na wanamgambo wa Hamas.

Marekani kwa mara ya kwanza imeonyesha kugadhabika na kuitaka nchi hiyo yenye jeshi lenye nguvu kufikiria upya na operesheni yake kwa sababu watu wengi wasio na hatia wanapoteza maisha.

Hata hivyo, Ukanda wa Gaza jana usiku bado ulishuhudia mashambulizi makali kutoka kwa vikosi vya Israel na kusababisha mawasiliano ya simu kukatika.

Kampuni kubwa za mawasiliano katika eneo hilo Paltel na Jawwal, zilisema kuwa huduma zote za simu na intaneti zilikatika.

Mji wa Rafah ulioko mpakani na Misri ulishambuliwa usiku wa kuamkia jana.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamini Netanyahu, alisisitiza jana kwamba hawatasitisha vita hadi lengo lao la kuwasambaratisha Hamas linafikiwa.

Alimueleza mshauri wa masuala ya usalama wa Marekani Jake Sullivan, kuwa Israel itaendeleza vita vyake dhidi ya Hamas hadi wapate ushindi kamili.

Sullivan alijibu kauli hiyo kwa kueleza kuwa Marekani inataka kuona matokeo mazuri kuhusu nia ya Israel ya kuepusha madhara kwa raia.

Kwa mujibu wa taarifa ya serikali mjini Tel-Aviv, Netanyahu na Sullivan walizungumzia kuhusu vitisho vya kikanda ikiwa ni pamoja na kundi la Hezbollah la nchini Lebanon na waasi wa Houthis kutoka Yemen.

Pia walijadili juhudi za kuwaokoa mateka zaidi wanaoshikiliwa na Hamas pamoja na suala la kuongeza misaada ya kibinadamu kwa raia wa Gaza.

Sullivan alitarajiwa jana kufanya mazungumzo na rais wa mamlaka ya Palestina, Mahmoud Abbas, kujadili mipango baada ya vita kumalizika Ukanda wa Gaza.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na Sullivan inaweza kujumuisha kuanzishwa tena kwa vikosi vya usalama vya Palestina ambavyo vilisambaratishwa na kundi la Hamas mwaka 2007.

Kwa upande wake Waziri Mkuu wa Palestina, alisema katika mahojiano kuwa utawala wa Biden unatakiwa kuchukua hatua muhimu na kuishinikiza Israel kuelekea suluhisho la serikali mbili.

Hata hivyo, Israel ilisema kuwa wakati wa sasa sio wa kujadili suluhisho kama hilo.

Katika hatua nyingine, Israel ilitoa taarifa kuwa wanajeshi wake 116 wamekufa tangu kuanza kwa operesheni hiyo ya ardhini maeneo ya Ukanda wa Gaza baada ya Hamas kuvamia kusini mwa Israel Oktoba 7 na kuua watu wapatao 1,200 na wengine 240 walichukuliwa mateka. Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant, alieleza kuwa itachukua miezi kadhaa kuwashinda kundi la Hamas.

Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, alimwambia Rais wa Marekani, Joe Biden, kwamba ana jukumu la kihistoria la kufikia haraka makubaliano ya usitishwaji wa mapigano.

Erdogan alionya kwamba mashambulizi ya muda mrefu ya Israel huko Gaza yanaweza kuwa na matokeo mabaya duniani kote.

**DW**




Polisi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wakifuatilia wafuasi wa chama tawala katika moja ya mikutano ya kampeni inayoendelea nchini humo. **PICHA: AFP**

# Wasiwasi watanda uchaguzi DRC

**KINSHASA,** DRC

MWENYEKITI wa Tume ya Uchaguzi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (CENI), Denis Kadima amewaruhusu wapiga kura wote waliosajiliwa katika daftari kushiriki katika uchaguzi mkuu utakaofanyika wiki ijayo.

Alisema hata watu ambao kadi zao za kupigia kura zimeharabika wataruhusiwa kuingia katika vyumba vya kupigia kura.

Kuali hiyo ya CENI imeungwa mkono na mahakama ya katiba ambayo imekataa madai ya kuahirisha uchaguzi yaliyotolewa na wagombea urais wa upinzani kutokana na taratibu kupindishwa.

Mahakama ilisema katika hukumu kuwa madai yao hayana msingi na mchakato wa uchaguzi utaendelea kama ilivyopangwa.

Kumekuwa na wasi wasi kuwa idadi kubwa ya wapiga kura huenda wasishiriki uchaguzi baada ya maelezo kwenye kadi zao kufutika.

Tume ya uchaguzi iliendesha shughuli ya kuwapa wapiga kura waliosajiliwa kadi mpya baada ya zile za awali kuharibika.

Hata hivyo, zoezi hilo limekuwa likienda pole pole kutokana na idadi kubwa ya watu waliojitokeza ili kubadilisha kadi.

Kadima aliongeza kuwa hadi sasa hawajafanikiwa kupata ndege za kutosha kusafirisha vifaa vitakavyotumika wakati wa uchaguzii maeneo yote.

Siku mbili zilizopita CENI iliiandikia serikali ya DRC na Umoja wa Mataifa kuomba msaada wa kupatiwa ndege ili kufanikisha shughuli ya kusafirisha vifaa vya kupigia kura.

Kumekuwa na wasi wasi kuwa idadi kubwa ya wapiga kura huenda wasishiriki baada ya maelezo kwenye kadi zao kufutika.

**BBC**



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, akikabidhiwa tuzo na Mkurugenzi Mtendaji wa PSPTB, Godfred Mbanyi, baada ya kufunga Kongamano la 14 la Mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi, jijini Arusha jana. **PICHA: LUSUNGU HELELA**

# Serikali yajivunia mfumo wa kidijitali ununuzi wa umma

**Na Lusungu Helela,**
ARUSHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amesema ununuzi wa umma umekuwa ukiripotiwa kugubikwa na rushwa na ubadhirifu na kwamba zaidi ya asilimia 72 ya bajeti ya serikali imekuwa ikitumika katika eneo hilo.

Kutokana na uzito huo, amesema serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) imeamua kusanifu, kujenga na kusanikisha Mfumo wa Kitaifa wa Kielektroniki wa Ununuzi Tanzania {National e-Procurement System of Tanzania (NeST)} ili kukabiliana na changamoto hiyo.

Kikwete alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati akifunga Kongamano la 14 la Mwaka la Wataalam wa Ununuzi na Ugavi. Kongamano hilo linashirikisha zaidi ya wataalamu 900 likiwa na kaulimbiu "Mabadiliko ya Kidijitali kwa Ajili ya Kuboresha Usimamizi na Ugavi Kuelekea Maendeleo Endelevu."

Amesema mfumo huo utasaidia kuondoa mianya ya rushwa na upendeleo, hivyo thamani ya pesa za Serikali katika bidhaa na huduma italindwa kwa kuwa kutakuwa hakuna ulazima wa watu kukutana ana kwa ana

"Ni furaha yangu kama Naibu Waziri ninayeshughulikia utawala bora ambapo ninasimamia uzuiaji na mapambano dhidi ya rushwa, naamini mfumo huu utaondoa hisia hasi zilizojengeka katika jamii kwenye suala la ununuzi wa umma, hivyo kuongeza uwazi," alisema.

Kikwete alisema mfumo huo utaongeza ufanisi, uwazi na ushindani katika ununuzi wa umma.

Katika hatua nyingine, Kikwete alisema serikali haitamvumilia mtu yeyote atakayesababisha upotevu wa rasilimali za nchi huku akiwataka wasithubutu kucheza na mfumo huo mpya wa ununuzi kwa umma.

Pia alitoa wito kwa waajiri wote kuhakikisha wataalam wa ugavi na ununuzi wanasajiliwa na wanazo sifa za kufanya kazi za ununuzi na ugavi ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kupitia mfumo.

# Eneo la malezi ya watoto latengwa Machinga Complex

**Na Julieth Mkireri**

UONGOZI wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salam kwa kushirikiana na Shirika la UN Women umetenga eneo kwa ajili ya malezi salama kwa watoto wa wafanyabiashara kwenye jengo la Machinga Complex.

Ukamilishwaji wa eneo hilo utazingatia mpango wa serikali jumuishi wa makuzi na malezi ya watoto.

Ofisa Maendeleo ambaye pia ni Mratibu wa Mradi kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Georgis Assenga, aliyasema hayo jana katika taarifa yake sokoni hapo ikiwa ni sehemu ya ziara ya Naibu Waziri na Katibu wa Nchi, Maendeleo ya Kimataifa wa Finland, Pasi Hellman, na ujumbe kutoka serikali ya Finland.

Alisema mradi huo ambao unatekelezwa na Shirika la UN Women kwa ufadhili wa Serikali ya Finland umefanikisha kutenga eneo hilo maalum la kulea watoto.

Georgis alisema kituo hicho kitatoa huduma pia, kwa wafanyabiashara wanawake kutoka masoko ya Mchikichini, Ilala, Kidongo chekundu na Kariakoo.

Alisema pamoja na vikwazo mbalimbali wanavyopitia wanawake wajasiriamali sokoni, ni kutokuwa na sehemu maalum ya kuangalia watoto wadogo.

Eneo hilo la kulelea Watoto, alisema lilitengwa kupitia Mradi wa Uongozi na Haki za Kiuchumi kwa Wanawake (Women's Leadership and Economic Rights Project - WLER), litawaruhusu wafanyabiashara wanawake kwenye soko kujitolea muda zaidi katika shughuli za kujiingizia kipato.

Alisema baada ya kufanikisha kutatua kikwazo hicho kilichokuwa mzigo kwa wafanyabiashara wanawake, kwa sasa wanatarajia kupitia mradi huo kuweka dawati la jinsia katika soko kusaidia kutoa elimu kuhusu haki za wanawake, kuzuia na kutoa msaada kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia.

Alisema wadau 300 pamoja na wanawake katika mitaa 19 katika kata nne kupitia mradi huo, wamenufaika na elimu ya wanawake kushiriki kwenye uongozi na nafasi za kutoa uamuzi katika ngazi mbalimbali, haki za kiuchumi na umuhimu wa kazi za matunzo na malezi zisizo na malipo.

Alisema elimu ya kutokomeza unyanyasaji wa kijinsia imetolewa kwa wanawake wiongozi wa serikali za mitaa na kata, watu maarufu, wanawake wenye ulemavu na wasichana wenye umri wa miaka 18 hadi 35.

Balozi wa Finland Nchini, Theresa Zitting, alisema wataendelea kuunga mkono kazi za kukuza na kuimarisha uongozi wa wanawake, kuwawezesha kiuchumi, na kazi zinazotokomeza ukatili kwa wanawake. Aliwahamasisha wanawake kuboresha kiwango cha bidhaa zao ili wauze zaidi.


**KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA**

**INGIAHEDI CHEDIEL MDUMA** anatangaza kupotea Kwa ofa ya kiwanja **No. 27314-DLR PLOT. 71 BLOCK J KISASA EAST-** Dodoma Municipality. yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **PHQ/DOD/DOD/9204/2023.**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**WALEED SULEIMAN SOUD**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye usajili namba MC 809 CKF. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi Taafifa: **PHQ/KIL/HAI/6348/2023**

**FOR SALE IN ARUSHA**

**Bitumen PG70-22 Sealed drums**

**Contact: 0767020869**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya................Kilolo**
**Kituo cha ..........Mahenge**
**Mkoa ..........Iringa**
**Usimamizi wa mirathi Na. 1 /2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU:**
**ABDALAH .S.BIN HYEJAN......... MAHENGE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA.......1 / 2022.......**

**TANGAZO**
**[kanuni ya 5{2} ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo]**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslah yioyote na mirathi yamarehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kujakuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 mwezi 12 mwaka 2023. kabla huyo mwombaji ajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia,**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukagukiwa.
Imetolewa leo tarehe 06....mwezi 12 mwaka ..2023...

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**EDSON FREDRICK ANDREA** anatangaza kupotea Kwa kadi ya pikpiki yenye jina MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD namba za usajili MC 161 DHK. aina ya BAJAJ BOXER, Chassis No. MD2A21BX1NWM92132, Engine No. PFXWNM21081. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/183035/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......131/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YAMAREHEMU:**
**MAUA ABDALLAH wa KAUZENI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA JAMILA AMIRI MOHAMED**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

**Imetolewa leo tarehe 7 mwezi 12 mwaka 2023**

HAKIMU

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 25511 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE NATHAEL GOMBE SIAFU**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY LAWRENCE SIAFFU SEMPEHO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of administration is made to the above named petitioner. Objection to the grant should be filed on or before the 15th day of January, 2024.
**DATED** at **KOROGWE** this 15th day of December, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

# HADITHI

# MAMA MWENYE NYUMBA - 6

MWANTUMU, au mama Mwadawa, ni mwanamke ambaye muda wote yeye anachowaza ni umbea, ugomvi na kufitinisha watu. Anawagombanisha majirani wasielewane, ndoa za majirani zake nazo haziko salama hajaziacha, kwani amekuwa akizitikisa. Kwa bahati mbaya au nzuri anaishi kwenye nyumba ya urithi ya marehemu mama yake, yeye akiwa ndiye mama mwenye nyumba. Cheo hicho cha Umama wa Nyumba asiyojenga, ndiyo akawa amepata fimbo ya kuwapigia watu. Wapangaji wanaopanga kwenye nyumba hiyo wamekuwa wakiishi kwa amri, manyanyaso, kufokewa kama watoto wadogo. Ndani ya nyumba hiyo, wapangaji wamekuwa kama wakiishi bure au kwa mama wa kambo, huku silaha yake kubwa ikiwa ni kuwatishia kuwahamisha. Hebu fuatilia mwanzo na mwisho wa visa vya mama huyu.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Wapangaji wake walionekana kumdharau na kumjibu kila wanachojisikia kujibu.

Kwa ile sauti alivyoipandisha, Devota na Tabia waliangua vicheko kila mmoja chumbani mwake kama wameambizana vile.

"Tunasubiri kodi iishe tu dada, nani anataka tena kukaa kwenye kijumba chako hiki kibovu na mvua hizi. TV yangu imeingia maji nimekwenda kuitengeneza, shilingi elfu ishirini zimenitoka, mwenyewe nimezipatia tabu nimetoka kudanga huko, narudi nakuta nyumba yote inavuja, TV kila nikiwasha wapi. Pesa ya kudanga ikabidi nimpelekee fundi inahusu." Bado Tabia alizidi kupiga kwenye mshono.

Wakati huo mama mwenye nyumba akaona ameuwasha moto na hawezi kuuzima, wapangaji wamemchachamalia. Akaamua kuingia ndani kimya kwa hasira. Akaazimia kuwa kesho atakwenda kumuona dalali aanze mipango ya kusaka wapangaji wengine baada ya waliopo kumaliza mikataba yao.

************************

"Haya haya amkeni, aliyechukua fagio langu hapa nani?" Ilikuwa ni sauti ya Rozi. Ni mmoja wa wapangaji ambaye mara nyingi mchana hayupo kwa sababu anafanya kazi saluni.

"He, makubwa, jamani hata fagio la shilingi elfu moja tu humu ndani mnashindwa kununua, kama maisha yamewashinda si mrudi kijijini tu."

"We mtoto we acha dharau, usitupigie kelele wengine bado tumelala, si uwaulize hao wapangaji wenzio, unatuchanganya wote kwa nini? Hapa kila mtu ana fagio lake." Mama mwenye nyumba alitoka ndani khanga mkononi kujibu tuhuma.

"Bibi eee, wala sijakutaja, unajishuku, mimi nimeuliza kwa wote." Rozi akarudisha jibu.

Utaratibu wa ndani mle ni kwamba kila mpangaji ana fagio lake la kufagia uwanja, na ule wa kufanyia usafi msalani.

Ni kwa sababu hawaishi kwa amani, mara nyingi wanaishi kinafiki kutokana na mama mwenye nyumba kufanya kazi ya kuwafitinisha




**"Usitake kunifanya mimi mjinga. Mimi nina akili. Mbona sijakuuliza wengine?"**

mara kwa mara.

"Kwa sababu fagio silioni, basi leo sifagii nawaambia ngoja niondoke zangu." Ulikuwa uamuzi wake baada ya kushindwa kuupata ufagio.

"Jamani, unajua nimechoka, visa vya nyumba hii vimenichosha kabisa, ngoja tu kodi yangu iishe nijiondokee, maana, najuta kabisa kupanga nyumba kama hii, yaani huyu dalali aliyenileta hapa nitamlaani siku zote."

Rozi alichukua ndoo yake ya maji ya kuoga, akaingia bafuni. Alipotoka alipatwa na mshangao.

Alichokiona mbele yake ni ule ufagio aliokuwa akiusaka na kuuliza watu upo pale alipokuwa amesimama awali akiuulizia.

"Haya huu umetoka wapi? Ulipandishwa na kushushwa kutoka mbinguni?" Akauliza.

"Ufagio wangu nimeupata lakini narudia tena kuwa sifagii, tayari nimeshaoga, mlitaka kuniibia ufagio wangu mmeshindwa, nifagie saa hizi, kijua kimeshaanza kutoka, nimeshaoga, maji yenyewe ya shida, nikachukue tena maji nikaoge, tutaonana kesho, na kuanzia leo nauweka ndani, hadi uchakae ndiyo nautoa, najua tu mliuchukua kwa sababu bado mpya nimeununua juzi tu," akasema huku akiuchukua ufagio wake na kuingia nao ndani.

Dakika mbili tu baadaye, wakati Rozi anajipamba, akashtukia mtu anaingia kwa kunyata na tahadhari kubwa. Alikuwa ni mpangaji mwenzake Tabia.

"Nikwambie, aliyechukua ufagio wako ni mama mwenye nyumba wako." Akaongea kwa kunong'ona ili sauti isiende mbali.

"Kumbe umemuona alipouchukua?"

"Hapana, nimemuona wakati anaurudisha. Ulipoingia bafuni tu. Akafungua mlango mama, akachungulia, alipoona hakuna mtu anayetoka, wala aliye nje, akatoka upesi na ufagio, akaenda kuuweka chini pale taratibu ili kishindo kisisikike, akarudi ndani kwake upesi upesi akafunga na mlango. Ila usinitaje mwenzako, maana mimi ndiye hanipendi kabisa, katika wapangaji wake wote mimi ndiye adui yake namba moja," Tabia alimpa umbea na kumtahadharisha Rozi.

Naye akatoka kwa kuchungulia na kunyata. Alipoona hakuna mtu anayemuona akatoka upesi akijaribu kukimbia, lakini kwa kuchuchumia ili miguu yake isitoe vishindo.

Alichelewa na wala haikuwa kama alivyotaka. Mwantumu alimuona. Na akajua kabisa kuwa kapeleka umbea. Mbona kazi ipo!

**********************************

"Enhe niambie, una uhusiano gani na mama mwenye nyumba?"

"Mama mwenye nyumba?"

"Unajifanya unashangaa, wakati mlikuwa wote!"

"Wapi?"

"Usitake kunifanya mimi mjinga. Mimi nina akili. Mbona sijakuuliza wengine?"

Jamaa akabaki kimya. Lakini alikuwa na uhakika kuwa nini mkewe alikuwa anakiongea.

"Wewe majuzi hukuwa na Mwantumu kule Magomeni Uwanja wa Barafu? Asubuhi ile mlikuwa mnaongea nini?"

"Ahaa, nimeshakumbuka, alikuwa ananiambia kuhusu ugomvi wake na wewe, anasema yeye hataki kutuhamisha, ila nikae na wewe nikwambie muelewane tu."

Yalikuwa ni malumbano ya Devota na mmewe. Siku ile mama mwenye nyumba alipomfuata kwenda kuongea naye, kuna watu waliwaona na wakapeleka mrejesho kwa mkewe.

Mume wa Devota alikumbuka maongezi yote waliyoongea siku hiyo, lakini akaamua kuyachuja ili asilete mtafaruku.

Alikuwa na uhakika pamoja na kwamba kuna mtu au watu waliowaona, lakini hakusikia walichoongea.

"Hivi wewe nawe, unaweza kusimama vipi na huyu mama mwenye nyumba peke yenu, mtu ambaye hana mume?"

"Huyu ni mama mwenye nyumba wetu ujue Devota."

"Hata kama, lakini mazoea yakizidi mwisho mnajenga mahusiano. Na kwa nini mjifiche huko? Mambo ya nyumbani si yangezungumzwa hapa? Au unabisha nimfuate nikamwambia aache kusimama na wanaume za watu njiani?"

ITAENDELEA JUMAMOSI

# BARTHEZ KOCHA MPYA WA MAKIPA FGA TALENTS

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa zamani wa klabu ya Yanga, Ali Mustapha 'Barthez', ametangazwa kuwa kocha mpya wa makipa wa timu ya Fountain Gate Academy Talents inayoshiriki 'Championship'.

Akizungumza jana kutoka Morogoro yalipo Makao Makuu ya klabu hiyo, Barthez, alisema ana furaha sana kujiunga na timu hiyo na akaahidi atafanya kazi yake ya kuwafundisha makocha ipasavyo.

"Niliipokea taarifa hii ya kuchukuliwa na FGA Talents kwa furaha kwa sababu ni timu yenye malengo, nikaona nitafanya kazi na watu ambao wanajua nini kinahitajika kwenye mpira, nadhani kuna kitu kitaenda kupatikana kwenye timu, hata huku Kocha Mkuu Ngawina Ngawina nimeshafanya naye kazi na hiki ni moja katika ya vitu vilivyonivutia kufanya naye kazi kwa mara nyingine," alisema.


Alisema katika klabu hiyo kazi yake itakuwa ni kupunguza makosa ya makipa ambayo yameonekana kwenye mechi za ligi hiyo zinazoendelea.

**"Kazi yangu itakuwa ni kupunguza makosa ya makipa, shida yao ni nini na kuwafanya waanze kupata 'clean sheets' na kuifanya timu sasa ianze kupa ta matokeo mazuri," alisema.**

Wakati Barthez alipewa kazi hiyo, klabu hiyo imemtangaza Ngawina Ngawina kuwa Kocha Mkuu akichukua nafasi ya Athumani Cairo aliyetimuliwa hivi majuzi yeye na msaidizi wake Boniface Kiwale baada ya mfululizo wa matokeo mabovu ya mechi za ligi hiyo.

Barthez alizichezea pia timu za Mogo FC ya Karakata, Pentagon, Mkunguni, Kumbukumbu, Ashanti United iliyokuwa Ligi Kuu wakati huo na Simba kabla ya kujiunga na Yanga na sasa amegeukia ukocha.

Ngawina, ameshawahi kuichezea klabu ya Kahama United, Kariakoo ya Lindi kabla ya kutimkia nje kucheza soka la kulipwa katika klabu za Mukura Victory ya Rwanda na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.




Meneja wa wateja maalum wa tigopesa, Mary Rutta (kushoto) akimkabidhi mfano wa hundi ya Shilingi milioni tano, Janeth Mgweno mshindi wa magifti dabodabo jana. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Watatu washinda pesa magifti dabodabo

**Na Mwandishi Wetu**

WATU watatu wakazi wa Dar es Salaam wameibuka washindi wa pesa katika droo ya nne ya kampeni ya magifti dabodabo inayoendeshwa na kampuni ya tigo.

Luhuvilo Magombola Mkazi wa Mabibo, David Bombeki mwanafunzi wa chuo cha DIT na Janeth Mghweno Mkazi wa Shekilango wameingia kwenye orodha ya washindi wa kampeni hiyo.

Luhuvilo na David wameshinda Shilingi milioni moja huku Janeth akiibuka mshindi wa Shilingi milioni tano bna kufanya idadi ya washindi mpaka sasa kufikia 50 tangu kuzinduliwa kwa kampeni hiyo mwishoni mwa mwezi uliopita.

Akizungumza baada ya kuwakabidhi mfano wa Hundi washindi hao, Meneja wa Wateja Maalum wa TigoPesa Mary Rutha amewasisitiza Watanzania kuendelea kufanya miamala mbalimbali na Tigo Pesa ili kuibuka washindi katika kampeni hiyo.

"Muda huu tunaozungumza kuna washindi 15 wanarudi leo hii kutoka DUBAI, na wengine wamerudi jana kutoka Zanzibar lakini bila kusahau kuna wengine wamejishindia Pesa taslimu na wapo pia waliojishindia Vifaa vya Hisense kwa hiyo kampeni bado inaendelea fanyeni miamala na TIGO PESA kwa wingi, Lipa kwa Simu, nunua vifurushi ili utengeneze mazingira ya kuibuka Mshindi " alisema Mary.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti washindi hao wameipongeza kampuni ya tigo kwa kuwakumbuka wateja wake kupitia kampeni hiyo.

"Nawashukuru sana Tigo.., sikuamini nilipopigiwa simu kuwa nimeshinda milioni tano, sikuamini mpaka nilipokuja hapa kwenye ofisi zao kukabidhiwa, pesa hii itanisaidia sana," alisema Janeth mshindi wa shilingi milioni tano.

## Namungo kufanya usajili wa kishindo

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Namungo FC umesema utafanya usajili wa kishindo msimu huu ili kuimarisha zaidi timu yao.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Ally Mkadeba alisema watasajili wachezaji ambao wataleta mafanikio na si ukubwa wa majina kwa kuwa wamepania kuimarisha timu yao ili iweze kufanya vizuri kwenye ligi.

"Tutafanya usajili wa kishindo tukiwa na malengo ya kushika nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ili kuwapa burudani mashabiki wetu", alisema Mkadeba.

Katibu huyo alisema wataanza usajili huo mara baada ya kupokea na kupitia ripoti ya aliyekuwa Kocha wao Mkuu Denis Kitambi ambaye kwa sasa amejiunga na Geita Gold.

Aliongeza kuwa kwa sasa wanaelekeza nguvu zao kwenye mchezo wa leo wa Kombe la Shirikisho la Azam (FA) dhidi ya Holly wood FC ya Songwe mchezo ambao utapigwa kwenye uwanja wa Majaliwa.

Kwa sasa timu hiyo ipo chini ya kocha msaidizi Shadrak Nsajigwa ambaye anaisimamia timu hiyo mpaka pale atakapopatikana kocha mpya atakeyechukua mikoba ya Kitambi.

Nsajigwa aliiambia Nipashe jana kuwa wachezaji wapo na morali ya juu licha ya kuondoka kwa kocha Kitambi na baada ya mchezo wao wa FA watakutana na Tanzania Prisons kwenye mchezo wa ligi kuu.

## Wawili kushiriki Gofu Afrika

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI wawili wa Tanzania Madina Idd na Vicky Elius wanatarajiwa kushiriki mashindano ya riadha ya gofu ya Afrika yatakayofanyika nchini Afrika Kusini Februari mwakani.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Mashindano wa Chama cha gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU) Hawa Wanyeche, alisema wachezaji hao wamepata nafasi hiyo baada ya kupata mualiko maalum.

"Wachezaji hawa wamepata nafasi hiyo baada ya kupata mualiko kutoka Afrika Kusini kila mchezaji anatamanikwenda kushiriki katika mashindano haya makubwa lakini ni wachezaji wawili tu waliopata mualiko kutoka kwa waandaaji," alisema Wanyeche.

Aidha, aliongeza kuwa endapo nafasi nyingine zikitokea wachezaji wengine watapata fursa ya kwenda kushiriki katika mashindano hayo kwa kuwa muda bado hupo wa kuomba kushiriki.

"Bado kuna nfasi ya muda, tutaendelea kuwasiliana na waandaaji kama kuna nafasi basi wachezaji wengi zaidi waende kushiriki katika mashindano haya," alisema Wanyeche

Katika hatua nyingine, Wanyeche alisema kwa sasa mchezo wagofu kwa wanawake unazidi kushika kasi na wanawake wengi zaidi wameanza kuuelewa

"Sasa hivi wanawake wameanza kuuelewa mchezo huu tofauti na miaka ya nyuma, washiriki walikuwa wanaume zaidi, lakini pia vyombo vya habari vimesaidia kuhamasisha kwa kiasi kikubwa huu mchezo mpaka sasa tunaona wanawake wengi zaidi wanajitokeza kucheza," alisema Wanyeche.

## ZISIKUPITE

**CASEMIRO ATAKIWA PSG**

KLABU ya Paris St-Germain ina nia ya kutaka kumnunua kiungo wa Manchester United na Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 31, ambaye pia amekuwa akihusishwa na klabu ya Al-Hilal ya Saudi Arabia. (***Sports Zone via Sun***)

**SANCHO BADO HAKIELEWEKI**

KLABU ya Manchester United inatatizika kupata mnunuzi wa mshambuliaji Mwingereza Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23, huku mshahara wake wa pauni 350,000 kwa wiki ukiaminika kuchangia hali hiyo. (***Sun***)

**MO SALAH NI NGUMU**

MKURUGENZI wa soka wa Ligi ya Saudi Arabia, Michael Emenalo anaamini kuwa itakuwa vigumu kumshawishi mshambuliaji wa Liverpool mwenye umri wa miaka 31 kutoka Misri, Mohamed Salah kujiunga na ligi hiyo Januari. (***Sky Sports***)

**DE GEA KUREJEA EPL**

GOLIKIPA wa zamani wa Manchester United, David de Gea mwenye umri wa miaka 33 kwa mara nyingine tena amechochea uvumi wa kurejea Ligi Kuu ya England kwa kuchapisha ujumbe kwenye mitandao wa kijamii. (***Mirror***)

**SOARES AWANIWA**

KLABU ya Villarreal inavutiwa na beki wa Arsenal, Cedric Soares mwenye umri wa miaka 32 raia wa Ureno. (***ESPN***)

**ANGE KUSAJILI BEKI**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou anataka kusajili beki mpya katika dirisha la uhamisho la Januari. (***Standard***)

**VARMEEREN AFUATILIWA**

KLABU za Arsenal na Tottenham Hotspur zilituma maskauti wao kumfuatilia kiungo wa Ubelgiji, Arthur Vermeeren mwenye umri wa miaka 18 akiichezea Royal Antwerp katika ushindi wao mnono wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona. (***90 min***)

**CARVALHO KUREJESHWA**

KLABU ya RB Leipzig imewasiliana tena na Liverpool ili kueleza nia ya kutaka kumbakisha winga wa Ureno, Fabio Carvalho mwenye umri wa miaka 21, licha ya Wekundu hao kumtaka arejee nyumbani kwa kukosa muda wa kucheza. (Fabrizio Romano)

**XAVI MAMBO MAGUMU**

KOCHA wa Barcelona, Xavi mwenye umri wa miaka 43 anakabiliwa na wakati mgumu uwanjani Nou Camp baada ya mfululizo wa matokeo mabaya, na hakuna mkuu wa bodi ya klabu hiyo anayemuunga mkono Mhispania huyo. (***AS***)

**PAEZA SAFI CHELSEA**

KIUNGO wa Ecuador mwenye umri wa miaka 16, Kendry Paez atafanya mazoezi na Chelsea wiki ijayo. The Blues walimsajili kutoka Independiente del Valle msimu uliyopita kwa makubaliano ya kujiunga na klabu hiyo atakapotimiza umri wa miaka 18. (***Telegraph***)



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# JEZI ZA MESSI ZAUZWA KWA MAMILIONI

**NEWYORK,** Marekani

### ●●● Ipo iliyotumika kwenye mchezo wa fainali za kombe la Dunia dhidi ya Ufaransa na....

JEZI sita ambazo Lionel Messi alivaa wakati wa kampeni ya kihistoria ya Kombe la Dunia 2022 ya Argentina, ikijumuisha moja ya ushindi wao dhidi ya Ufaransa kwenye fainali, iliuzwa kwa dola milioni 7.8 kwenye mnada wa hapa NewYork.

**Ofa tatu zilileta bei ya mauzo ya dola milioni 7.8 ikijumuisha malipo ya mnunuzi kwenye mnada wa Sotheby's New York.**

Jezi ambazo Messi alivaa katika kipindi cha kwanza kati ya mechi sita za Argentina nchini Qatar ziwekwa kwenye mnada na kampuni ya teknolojia ya AC Momento na zimeenda kwa mzabuni ambaye jina lake halikutajwa.

Licha ya matumaini kwamba bei yake ingeweka rekodi ya jumla, lakini ilikuwa pungufu ikilinganishwa na jezi iliyouzwa dola milioni 10.1 Septemba 2022 katika jezi moja ya Michael Jordan ya Fainali za NBA za mwaka 1998.

Jezi ya Diego Maradona "Hand of God", ambayo iliuzwa Mei 2022 ilinunuliwa kwa dola milioni 9.28.

Hata hivyo, bei hiyo ya kununuliwa kwa jezi za Messi ndiyo ya juu zaidi kwa kumbukumbu za michezo katika mnada mwaka huu na imeweka rekodi.

Kuelekea katika mnada huu, rekodi ya awali iliyotumika kununua jezi iliyovaliwa na Messi ilifikia dola 450,000 (zilizotumika Mei 2022) kwenye jezi aliyovaa akiwa na Barcelona kwenye El Clasico mnamo 2017.

Messi alikuwa nahodha wa Argentina wakati wakiishinda Ufaransa kwa mikwaju ya penalti katika mchezo wa fainali baada ya sare ya 3-3.

Mkusanyiko huo ulijumuisha jezi alizovaa Messi katika kipindi cha kwanza kati ya mechi mbili katika hatua ya makundi, ushindi wao wa 2-1 dhidi ya Australia katika hatua ya 16 bora, ushindi wao wa robo fainali ya mikwaju ya penalti dhidi ya Uholanzi, ushindi wa 3-0 dhidi ya Croatia nusu fainali, na ushindi dhidi ya Ufaransa kwenye fainali.

# KLOPP ARIDHIKA KIWANGO LIVERPOOL




**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp anaona mwelekeo mzuri wa Liverpool licha ya kufungwa 2-1 na Union Saint-Gilloise kwenye Ligi ya Europa, Alhamisi.

Ikiwa nafasi ya kwanza katika Kundi lake la E na tayari imefuzu hatua ya 16 bora, Klopp anaona maendeleo makubwa kwa kikosi chake.

Mohamed Amoura alianza kuwafungia wenyeji dakika ya 32, lakini Jarell Quansah akasawazisha kwa bao lake la kwanza kwa Wekundu hao dakika saba baadaye.

Na ingawa Cameron Puertas alifunga bao ambalo lilikuwa na ushindi kabla ya muda wa mapumziko, Klopp aliridhika na kile alichokiona.

Alisema: "Ulikuwa ushindi unaostahili kwa Union.

"Ingawa nilisikia sasa goli la kwanza linaweza kuwa la kuotea, hakuna anayeweza kusema vizuri. Tutaona hilo lakini nani anajali?

"Wamejipanga vizuri, wako juu ya msimamo kwenye Ligi Kuu ya Ubelgiji, walicheza vizuri n ani timu yenye nguvu zaidi..

"Tulihitaji kukua katika mchezo. Nina furaha sana kwamba ilitokea kipindi cha pili zaidi na zaidi na kwamba tuliupa mchezo mzuri.

"Kabla ya hapo, walitupatia mpira, wakashinda mipira kwenye shambulio la kushitukiza.

"Mwishowe, tungeweza kufunga bao la kusawazisha na ingekuwa vizuri. Tungependa kupata pointi hapa.

"Niliona maonesho mazuri. Tuliiacha na hiyo ni sawa kwangu. Hakuna mtu aliyejeruhiwa."

# Caicedo ataja sababu kuichagua Chelsea

**LONDON.** England

MOISES Caicedo amefichua kuwa ofa ya Liverpool "ilichelewa sana" kwenye dirisha la usajili, huku kiungo huyo akiwa tayari ameamua kuwa anataka kujiunga na Chelsea kufikia wakati huo.

Liverpool na Chelsea walikuwa kwenye vita vya kuwania saini ya Caicedo kutoka Brighton & Hove Albion wakati wa usajili wa majira ya joto.

Hatimaye alisajiliwa Stamford Bridge kwa ada iliyoweka rekodi mpya ya England ya pauni milioni 115.

Hapo awali Liverpool walikuwa wametoa ofa ya dau la pauni milioni 111 lililokubaliwa na Brighton kwa ajili ya mchezaji huyo.

Hata hivyo, katika mahojiano na Sky Sports, Caicedo amethibitisha kwamba alipendelea kujiunga na Chelsea kwa sababu walikuwa wameonesha nia ya kutaka huduma yake mapema.

"Nilikuwa nikizungumza na Chelsea kwa muda mrefu. Haikuwezekana kusema hapana kwa Chelsea, kwa sababu walikuwa nami wakiniunga mkono," alieleza.

"Katika majira ya joto niliteseka sana kwa sababu ilikuwa ngumu kuondoka Brighton. Walikuwa nami, na katika dakika ya mwisho Liverpool walinipigia simu lakini walikuwa

wamechelzea kwa sababu nilitaka kuichezea Chelsea."

Mambo hayajaenda sawa kwa Chelsea na usajili wao wa rekodi tangu uhamisho huo, huku kiungo huyo akihangaika kupata kiwango bora huku timu yhiyo ikiwa haikufanya vizuri.

Akizungumzia mwanzo wake wa maisha Stamford Bridge, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alikiri kwamba anavumilia "wakati mbaya" kwa sasa, lakini ana uhakika wa kurejea katika ubora wake hivi karibuni chini ya kocha Mauricio Pochettino.

"Kwa sasa, huu ni wakati mbaya kwangu, na familia yangu inateseka sana kwa sababu wanasoma na kusikiliza mambo ambayo watu wanasema juu yangu ambayo sio mazuri,"

alisema Caicedo.

"Ni ngumu. Ni ngumu kwangu, najaribu kuwa na nguvu, kwa sababu mpira wa miguu uko hivi, nimejiandaa kwa hili.

"Yeye (Pochettino) ananilinda dhidi ya ukosoaji. Amekuwa mkarimu sana na mvumilivu kwangu.

"Ananijua mimi ni nani na ndio maana anatulia nami. Niko hapa kwa miezi minne tu; sikufanya maandalizi mazuri ya msimu kwa sababu ilikuwa ngumu kwangu. Nina hakika nitaendelea vizuri."

# Mustakabali wa Varane Man United haujulikani

**MANCHESTER,** England

MKATABA wa Raphael Varane ndani ya Manchester United unamalizika mwishoni mwa msimu huu na sio msimu wa joto wa 2025 kama ilivyoaminika hapo awali, kwa mujibu wa 90min.

Mkataba wa Varane unajumuisha chaguo la miezi 12 kuurefusha hadi 2025, lakini ikiwa hautashawishiwa na klabu anaweza kuondoka Juni kama mchezaji huru.

Licha ya kutambulishwa kwa mbwembwe nyingi mwaka 2021, mustakabali wa Varane hapo Old Trafford uko mbali na uhakika, akiwa amepoteza nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza katika miezi ya hivi karibuni.

Harry Maguire amependekezwa kama beki wa kati anayeanza, huku pia ujio wa mkongwe Jonny Evans amekuwa sababu nyingine kwa Varane kuwa na wakati mgumu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 30 alijiunga na Man United kutoka Real Madrid kwa mkataba wa thamani ya zaidi ya pauni milioni 40, lakini mkataba mpya wakati huu unaonekana kutowezekana.

Iwapo United watachukua chaguo hilo kwenye mkataba wake wa sasa pia inatia shaka lakini klabu haijaikataa.

Zaidi ya Varane, United ina wachezaji kadhaa wenye majina makubwa ambao wanaweza kumalizika mikataba yao mwaka 2024.

Mchezaji mwenzake na Varane, Anthony Martial ni mmoja katika hali kama hiyo.

Mkataba wake unaisha mwaka 2024 na unajumuisha chaguo, lakini la kuongeza linaonekana kuwa gumu.

United pia inazingatia chaguzi walizonazo kwa safu ya ulinzi Victor Lindelof na Aaron Wan- Bissaka.

Wachezaji wote wawili mkataba wao pia unamalizika mwishoni mwa msimu huu.



# AUCHO KUWAKOSA, MTIBWA, TABORA UNITED, KAGERA SUGAR

**Na Adam Fungamwango**

KAMATI ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imekazia adhabu ya kiungo mkabaji wa Yanga, Khalid Aucho iliyotolewa katikati ya mwezi Novemba, baada ya kupitia maombi ya marejeo yaliyowasilishwa na klabu hiyo kuhusu adhabu hiyo.

Kamati hiyo chini ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), imesema imepitia maombi ya marejeo ya klabu ya Yanga na kwa mara nyingine imejiridhisha adhabu iliyotolewa ilikuwa sahihi.

**Taarifa iliyotolewa jana na kamati hiyo iliyokaa kikao chake Desemba 13, ambapo pamoja na mambo mengine ilipitia matukio mbalimbali ya ligi na kufanya maamuzi imeelezea Aucho ataikosa michezo mitatu ya ligi kuu.**

Mechi atakazozikosa ni dhidi ya Mtibwa Sugar utakaochezwa leo jijini Dar es Salaam, dhidi ya Tabora United utakaochezwa Desemba 22, ugenini na ule wa Desemba 26 dhidi ya Kagera Sugar utakaochezwa Uwanja wa Kaitaba mkoani Kagera.

Yanga iliwasilisha barua kuomba marejeo ya adhabu hiyo ikidai ni kubwa mno na ilikuwa ikiomba kupunguzwa.

"Kamati imejadili maombi ya marejeo ya klabu ya Yanga kushu adhabu ya kufungiwa michezo mitatu na kutozwa fainali ya shilingi laki tano iliyotolewa kwa mchezaji Aucho kupitia kikao cha kamati hiyo kilichoketi Novemba 14, hata hivyo, baada ya kupitia maelezo ya klabu ya Yanga na kanuni za ligi, kamati imejiridhisha kwa mara nyingine kuwa adhabu iliyotolewa kwa machezaji huyo ni sahihi, hivyo anapaswa kuendelea kuitumikia, ikimtaka kuzingatia mchezo wa kiungawa," ilisema sehemu ya taarifa hiyo taarifa hiyo.

Awali Bodi ya Ligi Kuu iliyokaa Novemba 14, ilimfungia Aucho michezo mitatu kwa kosa la kumpiga kiwiko mchezaji Ibrahim Ajibu wa Coastal Union, katika mechi uliofanyika Novemba 8, Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Yanga ikishinda bao 1-0.

## Simba yarejea nafasi ya tatu Ligi Kuu

INATOKA UK 24

bao la pili likiwekwa wavuni na Kanoute dakika ya 74, aliporuka juu na kuupiga kichwa mpira wa krosi kutoka wingi ya kushoto kwa Mohamed Hussein 'Tshabalala' ambaye naye alikuwa amepasiwa mpira wa kona fupi ya Ntibazonkiza.

Wakati kila mmoja akidhani mechi itaisha kwa mabao 2-0, Bocco, aliyeingia dakika kumi za mwisho kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Ntibazonkiza, alipachika bao la tatu dakika ya 89.

Bocco alifunga bao hilo akitumia vizuri makosa makosa ya beki wa kati, Mganda, Deus Bukenya alipomrudishia kipa Chalamanda mpira ambao haukuwa na kasi na Bocco kuuwai na kufunga bao hilo la tatu.

Baada ya mchezo huo, Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Mexime, alikubali matokeo na kusema makosa waliyoyafanya wachezaji wake yamewagalimu.

"Tumefanya makosa matatu na wenzetu wameyatumia kutuadhibu, wenzetu walikuwa bora zaidi leo na ndio sababu ya kufungwa," alisema Mexime.




Meneja wa Kampuni ya RTA Group, Kigambo Abdallah (katikati) akiwa na mwakilishi wa kampuni hiyo Reuben Bunini wakikabidhi jana sehemu ya msaada kwa Mlezi wa kituo cha watoto wenye uhitaji cha Msongola Dar es Salaam, Christina Haule. **PICHA: MPIGA PICHA WETU** .

# Namungo vinara wa penalti Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikirejea jana kwa mchezo kati ya Simba dhidi ya Kagera Sugar, na leo kati ya Yanga dhidi ya Mtibwa Sugar jumla ya penalti 13 zilikuwa zimetolewa huku Namungo ikiwa ndiyo timu inayoongoza kwa 'kuzawadiwa' penalti nyingi kuliko timu nyingine yoyote.

Kwa mujibu wa dawati letu la takwimu na zile zilizotolewa juzi na Bodi yaLigi Kuu jana inaonyesha kuwa Namungo imefanikiwa kupata penalti tatu mpaka sasa, ikiweka wavuni mbili na kupoteza moja.

Wakati Namungo ikiwa kinara wa kupata penalti nyingi, timu ya Simba na Coastal Union zinafuatia kila mmoja ikipata penalti mbili.

Timu zingine zilizopata penalti moja moja na kuzitumia ni Azam FC, JKT Tanzania, Kagera Sugar, Tabora United, Prisons, Yanga, huku Gaita Gold ikipata moja, lakini ikiipoteza kupitia kwa Elius Maguri aliyekosa katika mechi ambayo timu yake ilifungwa mabao 2-1 dhidi ya KMC.

Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya penalti 13 zilizopatikana mpaka sasa, 10 zimezaa mabao na penalti tatu zimeota mbawa.

Mbali na Maguri, wengine waliokosa ni Henock Mayala wa Coastal Union na Derrick Mukombozi wa Namungo aliyekosa katika mechi ambayo timu yake ilishinda mabao 2-0 dhidi ya Ihefu.

Wachezaji waliofunga penalti zao ni Fabrice Ngoye wa Namungo kwenye sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC, Jean Baleke wa Simba, ikiifunga Coastal Union mabao 3-0, Saido Ntibazonkiza wa Simba ilipochapa Prisons mabao 3-1, Daniel Lyanga wa JKT Tanzania ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Kagera Sugar, Erick Okutu wa Tabora United, iliyoshinda mabao 2-1 dhidi ya Dodoma Jiji, Mukombozi wa Namungo akifunga mechi ambayo timu yake ilifungwa mabao 3-2 dhidi ya Singida Fountain Gate, Lucas Kikoti wa Mtibwa aliyefunga dhidi ya Mashujaa wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0, Obrey Chirwa wa Kagera Sugar wakati walipoifunga Prisons mabao 2-1, Pacome Zouazoua wa Yanga wakati timu hiyo ikiibuka na ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Simba na Prince Dube wa Azam FC aliyefunga kwenye ushindi wa Yanga wa mabao 3-2.

## Gamondi: Sina presha na timu yangu, tupo tayari kwa Mtibwa

INATOKA UK 24

akifunga mabao saba.

"Timu imecheza michezo 18 imefunga mabao 40, viungo watatu wa juu wamefunga mabao 23 watu wanataka nibadili wachezaji nankutumia mawinga je kati ya viungo hao nani nimtoe na kuwapa nafasi mawinga?, alihoji Gamondi.



Aidha, alisema kwenye kiungo mkabaji analazimika kumpa nafasi Khalid Aucho kwa kuwa amekuwa akionyesha kiwango

# Michezo

Jumamosi Desemba 16, 2023

Nipashe




UK. 22

Klopp aridhika kiwango Liverpool



Mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza akipiga penalti na kuifungia Simba bao la kwanza kwenye ushindi wa mabao 3-0 walioupata jana dhidi ya Kagera Sugar kwenye uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. **PICHA: SALEHJEMBE**.

# Simba yarejea nafasi ya tatu Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

●●● Ni baada ya ushindi wa jana dhidi ya Kagera Sugar, Mexime afunguka huku....

MABAO ya nahodha John Bocco, Saido Ntibazonkiza na Sadio Kanoute jana yameirudisha Simba katika nafasi ya tatu, ikipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar jana kwenye uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Simba ambayo kabla ya mechi hiyo ilikuwa kwenye nafasi ya tano ya msimamo wa Ligi Kuu na pointi zake 19, imefikisha pointi 22 na kukwea hadi nafasi hiyo, ikiwa imezidiwa na timu mbili tu juu yake, Yanga inayocheza leo dhidi ya Mtibwa Sugar yenye pointi 22 na kinara wa ligi hiyo, Azam FC wenye pointi 28.

Hata hivyo, Simba ndiyo timu iliyocheza mechi chache zaidi, ikiwa imeshuka dimbani mara tisa tu, huku kama Yanga ikicheza leo itakuwa ni mchezo wake wa 10, huku Azam ikiwa imeshacheza mechi 12 mpaka sasa.

Ikiingia dimbani tangu Novemba 9 ilipocheza mechi ya Ligi Kuu kwenye uwanja huo huo na kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo FC, Simba iliandika bao lake la kwanza dakika ya nane lililofungwa kwa mkwaju wa penalti na Ntibazonkiza baaada ya yeye mwenyewe kuangushwa ndani ya eneo la hatari dakika ya tano.

Awali, kipa Ramadhani Chalamanda aliiokoa, lakini mwamuzi Hans Mabena na wasaidizi wake waliamua irudiwe kutokana na baadhi ya wachezaji kuingia ndani ya eneo la hatari kabla mpigaji hajafanya hivyo.

Penalti hiyo ilifungwa kiufundi na Ntibazonkiza akimuacha Chalamanda akienda upande wake wa kulia, mpira ukaenda kushoto na kuipa Simba bao la utangulizi.

**Baada ya bao hilo, Kagera Sugar walibadilisha mfumo wao wa kucheza wachezaji wengi nyuma ya mpira, badala yake wakajaza na kati na kutawala eneo la kiungo, na mechi ikaenda hivyo hadi mapumziko.**

Kipindi cha pili baada ya timu zote kufanya mabadiliko, mechi ilibadilika na kuwa ya kasi zaidi, lakini ni Simba iliyoonekana kukosa mabao mengi kupitia kwa Jean Baleke aliyeingia kipindi cha pili, Kanoute, Clatous Chama, Fondoh Che Malone na Ntibazonkiza.

Dakika ya 50, Chama alipiga shuti la chini lililompita Chalamanda, lakini beki Abdallah Mfuko aliuondoa kabla haujavuka mstari wa goli.

Anwar Jabir, nusura aipatie Kagera Sugar bao dakika ya 62, alipowahadaa na kupita katikati ya mabeki, Che Malone na Henock Inonga, lakini shuti lake lilipita juu ya lango.

Katika mechi ya jana, kipa wa Kagera Chalamanda alikuwa shujaa kwa kuokoa michomo mingi ya wachezaji wa Simba, huku Ayoub Lakred akiwa likizo kwa muda mwingi wa mchezo.

Baada ya kosakosa nyingi, hatimaye Simba iliandika

INAENDELEA UK 23

## Gamondi: Sina presha na timu yangu, tupo tayari kwa Mtibwa Sugar

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema hana presha na timu yake kuelekea mchezo wa leo wa ligi kuu Tanzania bara dhidi ya Mtibwa Sugar kwa kuwa wamejiandaa vya kutosha.

Yanga leo inashuka dimbani ikiwakaribisha Mtibwa Sugar katika mchezo wa Ligi Kuu utakaochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Akizungumza na Nipashe, Gamondi, alisema baada ya kurejea kutoka Ghana kwenye mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika, walipata muda wa kupumzika na kuiandaa timu kuelekea mchezo wa leo.

Alisema wamefanya maandaliz ya kutosha na kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo muhimu.

"Kikosi kipo tayari kuwavaa Mtibwa Sugar wachezaji wangu wapo katika hali nzuri, naamini tutafanya vizuri kwenye mchezo wa kesho," alisema Gamondi.

Katika hatua nyingine, Gamondi amesema kenye kikosi chake wanaofanya vizuri mazoezini na kwenye mechi ndio wanaopata nafasi ya kuana katika michezo mbalimbali.

Alisema wapo watuwanaotaka afanye mzunguko wa wachezaji lakini yeye anaangalia uwezo wa mchezaji na kile anachokitoa katika kila mchezo anaocheza.

"Mimi naangalia juhudi za mchezaji, ukiangalia viungo wamekuwa wakifanya vizuri na kufunga idadi kubwa ya mabao kuliko washambuliaji, wanafanya kazi nzuri na ndio sababu naendelea kuwapa nafasi mchezaji kama Maxi Nzengeli, Pacome na Aziz Ki," alisema Gamondi.

Alisema wachezaji hao watau kwa pamoja wamefunga mabao 23 katika michezo yote ya Yanga msimu huu huku Nzengeli akifunga mabao nane sawa na Aziz Ki huku Pacome

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >